SUPA JACKPOT
TZS. 1,159,574,731
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Jumatano Oktoba 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581453
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 9
**Mlinzi** wa watawa adaiwa kuua kwa risasi, ashikiliwa



UKURASA WA 19
**Malasusa** akemea wazazi kuwaacha watoto kujilea



UKURASA WA 19
**Moto** Kariakoo waibua hoja 2 mpya serikalini



# Katibu CWT, manispaa wavutana kurudi kazini

• **Ni** aliyeukataa ukuu wa wilaya; bosi wake adai hana barua... *Endelea ukurasa 3*




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Amiri wa Taifa la Qatar, Sheikh Tamim Bin Hamad Al-Than (wa nne kushoto) pamoja na viongozi wengine wa mataifa mbalimbali wakimwagilia miti maji, kuashiria ufunguzi wa mkutano wa kimataifa wa kilimo cha mboga na matunda, Doha juzi. **PICHA: IKULU**

## Mpango ataka ATCL kumaliza kero za abiria

UKURASA 2



Ndege mpya ya abiria aina ya Boeing 737- MAX9 yenye uwezo wa kubeba abiria 181 ikimwagiwa maji (water salute), baada ya kuwasili nchini kwa mara ya kwanza katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

## Wadau watoa maoni panga pangua ya Rais Samia

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA KUIVAA IHEFU KWA TAHADHARI** UK.24

**KATUNI** UK.6




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Prof. Said Aboud (kushoto waliokaa) na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, wakitiliana saini mkataba wa makubaliano ya ushirikiano wa kuboresha utafiti kwenye sekta ya afya jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni Mkurugenzi wa Taarifa za Utafiti na Masuala ya Udhibiti kutoka NIMR, Dk. Mary Meige (kushoto) na Meneja wa Kituo cha Mafunzo cha CCBRT, Regina Monyemangene. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango ataka ATCL kumaliza malalamiko ya abiria

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango, ametoa maagizo matano kwa Wizara ya Uchukuzi na Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ikiwamo kumaliza malalamiko ya abiria ya kuahirisha safari au muda wa safari kusogezwa.

Pia ametoa siku 14 kwa wizara hiyo na Wizara ya Fedha, kupeleka mapendekezo serikalini kuhusu gharama za usafirishaji wa mizigo ndani ya ndege hizo ambazo pia zinalalamikiwa kuwa kubwa.

Dk. Mpango alitoa maagizo hayo jana katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) wakati wa hafla ya kupokea ndege ya 13 aina ya B 737-Max 9 na uzinduzi wa ndege ndogo mbili za mafunzo ya urubani zilizokabidhiwa kwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

Alisema serikali imedhamiria kuwekeza katika sekta ya uchukuzi na kuongeza ndege zingine mbili zinazotarajia kuwasili nchini kati ya mwezi huu na mwisho wa mwaka na nyingine Machi, mwakani.

Dk. Mpango alitaja jambo la kwanza ni kuhusu utaratibu na usimamizi wa huduma za usafiri wa anga na kuelekeza wizara pamoja na Bodi ya Wakurugenzi ya ATCL kutimiza wajibu wao wa utoaji huduma ili kuimarisha ushindani wa kikanda na kimataifa na kuongeza mchango katika pato la taifa.

"Fanyeni kazi kibiashara kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kusimamia sekta. Tuhakikishe tunafikia malengo. Bado kuna malalamiko kwa ATCL kuhusu huduma za usafiri ikiwamo kuahirisha safari au kusogeza mbele muda wa kuanza safari.

"Kwenye kelele nyingi ni katika kiwanja cha Mwanza. Ninapendekeza baada ya kupokea ndege hii mpya matarajio ya Watanzania ni kuwa sasa shirika letu litamaliza kero hii ya kuwasubirisha au kufuta safari," alisema huku akiagiza wizara ifuatilie kwa karibu ubora wa huduma zinazotolewa na shirika hilo.

Pia alitaka ununuzi wa vyakula na viburudisho ndani ya ndege hizo, kipeumbele kiwe bidhaa zinazozalishwa nchini ambazo zimethibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kukuza kipato cha na ajira kwa wajasiriamali wazawa.

Agizo la pili ni kwa Bodi ya ATCL kulisimamia shirika ili kulinda mtaji uliowekezwa na serikali. Alisema serikali haitavumilia uzembe wowote utakaojitokeza kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

"Jambo la tatu, tumepokea changamoto ya gharama kubwa ya usafirishaji wa mizigo kwenda nje ya nchi na katika viwanja vyetu. Kiwanja hiki cha Julius Nyerere, Kilimanjaro na Karume kule Zanzibar ikilinganishwa na viwanja vya ndege vya nchi jirani lakini pia gharama za kusafirisha mizigo kwa kutumia ndege za mashirika mengine ya duniani.

"Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Fedha zishirikiane na wenzao wa Zanzibar ili kutambua na kubaini kiini cha changamoto hii na kupendekeza hatua zinazopaswa kuchukuliwa. " Hebu tazameni hizo tozo na kodi, mfanye uchambuzi wa kina na mlete mapendekezo serikalini," aliagiza.

Dk. Mpango alisema serikali imewekeza fedha nyingi kununua ndege hizo na kuboresha viwanja vya ndege na miundombinu yake kwa lengo la kuhakikisha shehena kubwa ya mzigo inapatikana na kuongeza mapato. Alitaka wafanyie kazi suala hilo na kupeleka mapendekezo kwa mamlaka ya serikali ya Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar na kuagiza hilo lifanyiwe kazi ndani ya siku 14 kuanzia jana.

Alisema ameridhishwa na hatua ya utekelezaji wa makubaliano ikiwamo kufanya tathmini ya awali ya kitaalamu ili kuandaa mikataba ya ujenzi ikiwa ni pamoja na tathmini ya sampuli za udongo kutoka eneo la mradi.

Makamu wa Rais aliitaka wizara kuhakikisha shughuli zote za awali zilizopangwa, zinakamilika ifikapo mwezi Februari mwaka 2024, ili uboreshaji na upanuzi wa jengo la abiria katika kiwanja cha Mwalimu Nyerere uanze rasmi. Jambo la tano, aliutaka uongozi wa NIT na marubani wakufunzi na marubani wanafunzi kutumia ndege za mafunzo walizokabidhiwa ili kutoa mafunzo kwa watu wengi.

Pia alimtaka Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, kukiangalia chuo hicho ili bajeti ya mwaka ujao wa fedha, kuyafanyika kazi maombi yake ya kuongezewa ndege mbili.

Aidha, alimtaka waziri huyo afanye kazi ya kuchambua maombi yaliyowasilishwa na ATCL kwa serikali kuweza kununua ndege ya pili ya mizigo na baada ya hapo kuyawasilisha serikalini.

Hata hivyo, Dk. Mpango alisema kukamilika uwekaji taa viwanja vya ndege vya Dodoma na Msalato utaongeza safari za ndege nchini. Pia alisema wameambiwa kuwa abiria wameongezeka kutoka 106,138 mwaka 2017 hadi kufikia milioni 1.7 mwaka 2022/23.

Waziri Mbarawa alisema huduma katika uwanja wa ndege wa Dodoma zinaanza kutolewa saa 24 kuanzia jana baada ya kukamilisha maboresho yake.

Mkuu wa NIT, Prof. Zecharia Mganilwa, alisema ndege mbili walizokabidhiwa zina uwezo wa kufundisha marubani watano kwa wakati mmoja, lakini uhitaji wa Watanzania katika masomo ya urubani, wameomba serikali iziongeze zingine mbili zenye injini moja na kukisaidia chuo kutoa mafunzo hayo kwa marubani 20 kwa mkupuo.

# Wadau watoa maoni panga pangua ya Rais Samia

**Na Christina Mwakangale**

WACHAMBUZI wa masuala ya kisiasa, wanasheria na wanasiasa wametoa maoni yao kuhusu uteuzi wa mara kwa mara unaofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ikiwamo wanataaluma kwenda katika nyadhifa za kisiasa.

Pia wametoa angalizo namna uteuzi unavyofanyika ndani ya kipindi kifupi huku wakishauri ufanyike upembuzi yakinifu ili mabadiliko yafanyike kwa muda mfupi pale inapobidi.

Naibu Katibu Mkuu Chama cha CUF Bara, Magdalena Sakaya, alisema ni miongoni mwa waliotoa maoni jana baada ya taarifa kutolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, kuhusu uteuzi na mabadiliko ya wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, makatibu tawala wa wilaya na Kaimu Kamishna wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

Katika uteuzi mpya na mabadiliko hayo yaliyofanyika jana usiku, Sakaya alisema liwekwe angalizo namna ambavyo wanataaluma waliochukua miaka kadhaa kujikita katika taaluma fulani, kupewa nafasi za kisiasa.

"Tutunze fani. Ukuu wa wilaya hauhitaji kwenda shule sana. Hata mtu wa kidato cha nne anaendesha tu ni namna ya kufanya mwingiliano na jamii, elimu, watoto na wazee. Ila wizara zingine zinahitaji fani. Maliasili, misitu, elimu huwezi kumpeleka mtu ambaye hana elimu.

"Mtu kama (William) Mwakilema ambaye amesomea mhifadhi, binafsi sijafurahia, ingawa naweza kupongeza mengine yote anayofanya Rais. Mtu amesomea shahada nne, leo akawe DC (mkuu wa wilaya)? Yako mashirika ya hifadhi ambayo yangemtumia lakini nani atamchukua akishateuliwa na Rais?" Alihoji.

Sakaya alisema Rais ni taasisi, hivyo ashauriwe namna ya kuteua wenye sifa kuepuka kufanya uteuzi na utenguzi wa viongozi wa umma ndani ya kipindi kifupi.

"Isijekuwa kuna watu wanamtumia Rais kwamba mama mtoe huyu, weka huyu kwa ajili ya mambo yao. Inabidi kuwa makini kwenye kuteua na isiwe kama mtindo kwa sasa," alisema.

Sakaya alisema wanataaluma waliosomea fani ngumu kama sayansi na uhandisi wawe tunu ya taifa kwa kutumiwa maeneo yenye mahitaji zaidi, ikiwamo kufanya utafiti na kuleta ufumbuzi wa changamoto.

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Abbas Mwalimu, alisema mabadiliko anayoyafanya Rais ni miongoni mwa malengo aliyojiwekea kwamba atafanya maridhiano na kurekebisha mifumo.

"Unapofanya mabadiliko yako ya aina mbili, yaani ya kitaasisi na watu. Unaangalia taasisi na majukumu yake ila kuna mabadiliko ya watu unaangalia nani anafaa wapi kulingana na sifa zake.

"Mtu ambaye alikuwa TANAPA anapelekwa Korogwe, huyu ni mtu ambaye anaifahamu jamii ya kifugaji kwamba mabadiliko hayo yanaangalia mtu huyu atatosha wapi," alisema.

Alisema jambo linalohitajika ni viongozi wanaoteuliwa kuwa wabunifu huku akibainisha kwamba uteuzi wa Rais uzingatie zaidi vijana kwa kuwa anataka fikra mpya kutoka kundi hilo ambalo ni zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema uteuzi alioufanya rais uko ndani ya mamlaka yake, ingawa bado nafasi za wanawake kwenye uongozi zimejificha.

"Kilichonishtua ni kwa Faki, yule alikuwa mtumishi wa umma. Inanipa wasiwasi kwamba wako viongozi ambao ni 'active politicians' na ni mtumishi wa umma. La pili, tunaangalia suala la jinsia. Ingawa Rais anajitahidi bado kuna changamoto za nafasi za wanawake, kuna haja ya kuongezeka," alisema.

**MABADILIKO**

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Rais amemhamisha kituo cha kazi Sixtus Mapunda kutoka Wilaya ya Sumbawanga kuwa Mkuu wa Wilaya ya Temeke akichukua nafasi ya Mobhare Matinyi, ambaye ameteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari - Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali.

Rais pia amemhamisha kituo cha kazi Mkuu wa Wilaya ya Urambo, Kenan Kihongosi, kwenda Momba mkoani Songwe, akichukua nafasi ya Fakii Lulandala, ambaye ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa UVCCM.

Aidha, Rais amemteua Elibariki Bajuta aliyekuwa Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) kuwa Mkuu wa Wilaya ya Urambo, Tabora.

Kadhalika, amemteua William Mwakilema, aliyekuwa Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA kuwa Mkuu wa Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, kuchukua nafasi ya Jokate Mwegelo ambaye ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT).

Katika uteuzi huo, Rais amemteua Nyakia Chirukile kuwa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Ngorongoro.

Rais Samia ametengua uteuzi wa Halfan Magani, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Korogwe na kumteua Goodluck Mwangomango, aliyekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Singida.

Wengine walioteuliwa ni Said Majaliwa kuwa Mkurugenzi wa Tanga Mjini, akitokea kuwa Mkurugenzi Wilaya ya Kilindi na Faraja Msigwa kuwa Mkurugenzi wa Kilindi. Kabla alikuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Karatu.

Naye Naima Chondo ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Singida huku Shamim Adam Sadiq, akiteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Ruangwa. Hamza Hussein Hamza ameteuliwa Katibu Tawala Wilaya ya Ngorongoro. Awali, Hamza alikuwa Ofisa Tarafa wa Ndugu, Kwimba mkoani Mwanza.

Aidha, Lameck Karanga Ngang'a, ameteuliwa kuwa Katibu Tawala Wilaya ya Karatu akipanda kutoka Katibu Tarafa Karatu kuchukua nafasi ya Msigwa huku Musa Kuji akiteuliwa kuwa Kaimu Kamishna wa Uhifadhi TANAPA. Awali alikuwa Naibu Kamishna wa Huduma za Shirika TANAPA.

# Katibu CWT, Manispaa Temeke wavutana uhalali kurudi kazini

**Na Mwandishi Wetu**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Temeke imesema hadi sasa Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Mwalimu Japhet Maganga, aliyeelekezwa kurejea katika kituo cha kazi cha kufundisha, hajafanya hivyo.

Kutokana na hali hiyo, Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Elihuruma Mabelya, amesema iwapo Maganga asiporejea kazini baada ya siku saba tangu alipotakiwa kufanya hivyo, hatua za kinidhamu zitafuata.

Septemba 23 mwaka huu, Mkurugenzi Mabelya alitoa tangazo kumtaka Maganga kurejea kwa mwajiri wake ifikapo Oktoba Mosi mwaka huu baada ya serikali kutokubali maombi ya kuendelea kuazimwa na CWT.

Katika tangazo hilo, inabainishwa kuwa Maganga aliomba kibali cha kuazimwa na CWT kwa mara ya kwanza Agosti 2017 kilichomalizika Septemba 30, 2020.

Maganga aliomba nyongeza ya kibali cha kuazimwa Juni Mosi 2020 na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi alimpa nyongeza Agosti 10, 2020 kilichoisha Jumamsoi iliyopita.

Katika tangazo hilo la Mkurugenzi, inaainishwa Maganga ambaye ana cheo cha mwalimu mwandamizi, aliomba tena kibali cha kuazimwa kwa mara ya tatu, lakini Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Utumishi hajaridhia.

Katika hali inayoonesha utata wa suala hilo, Rais wa CWT, Leah Ulaya, ambaye Katibu Mkuu ndiye mtendaji na msaidizi wake mkuu, anasema chama hicho hakijapokea barua inayomtaka Maganga kurejea katika kituo chake cha kazi, hivyo anaendelea na majukumu yake ya ukatibu.

Mkurugenzi Mabelya aliiambia Nipashe jana kuwa Maganga ni mtumishi wa umma, hivyo alitakiwa kuripoti kwenye kituo chake cha kazi Oktoba Mosi mwaka huu (Jumapili) kama alivyotakiwa katika tangazo.

Kuhusu msimamo wa ofisi yake kisheria, mkurugenzi alitamka: "Iwapo hataripoti kwenye kituo chake cha kazi kama alivyotakiwa kufanya hivyo, basi kanuni na taratibu za utumishi wa umma zitachukuliwa.

"Huyu ni mtumishi, siyo mtu wa CWT tena. Huyu ni mwalimu, anatakiwa kuwa kwenye kituo chake cha kazi.

"Tunahesabu hizo siku saba za kikanuni, baada ya hapo kama hajaripoti, tutafungua mashauri ya kinidhamu dhidi yake."

Mwandishi alipozungumza jana na Rais wa CWT, Leah, kuhusu suala hilo na namna walivyojipanga kujaza nafasi ya Katibu Mkuu, alisema kuwa hadi jana, walikuwa hawajapokea nakala ya barua inayomtaka Maganga kurejea kazini.

"Kwanza, sijajua ile nyaraka iliyoonekana ilikuwa ni barua au tangazo kwa sababu ili hatua zozote zichukuliwe ni lazima kuwe na mchakato halali ili kufanyia kazi.

"Suala la kibali ni mwajiri na mwajiriwa wake, na atamjulisha kwamba ninakubali uendelee au sikubali. Sasa mwajiriwa hajapata na wala sisi hatuna nakala. "Kwa hiyo, hatuwezi kufanya hatua zozote na sisi hatuna chochote tunachojua zaidi ya kujua kwamba ni Katibu Mkuu, ataendelea kuwapo na kazi zinaendelea," alifafanua.

Mwandishi wa habari hizi alipompigia simu Maganga kujua sababu za kutorejea kwenye kituo chake cha kazi, alipokea, lakini baada ya utambulisho na kuelezwa dhamira ya kupigiwa simu, alijibu kwa kifupi "nipo kwenye kikao" kisha akakata simu.

Mnamo Septemba 25, mwaka huu wakati wa kikao cha Baraza la Dharura la CWT jijini Dodoma, Nipashe ilizungumza na Maganga kuhusu suala hilo, akasema alikuwa hajapewa barua ya kukataliwa ombi lake la kuendelea kuazimwa na chama hicho.

Mwalimu huyo alichaguliwa Desemba mwaka jana na Mkutano Mkuu wa CWT kuwa Katibu Mkuu kuchukua nafasi ya Deus Seif. Awali alikuwa anatumikia nafasi ya Naibu Katibu Mkuu.

Januari 25 mwaka huu, Maganga na Makamu wa Rais wa CWT, Dinna Mathaman na Rais wa CWT, Leah Ulaya waliteuliwa na Rais kuwa wakuu wa wilaya, lakini ni Dinna pekee aliyekwenda kuapa kushika nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma.

Leah aliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe mkoani Geita wakati Maganga akiteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa mkoani Kagera. Wawili hao hawakwenda kuapa kutumikia nafasi walizoteuliwa na Rais.

# Mwili anayedaiwa kunyongwa nyumba ya wageni wazikwa

## ● Baba kwenda mahabusu kumwona mtuhumiwa

**Na Cynthia Mwilolezi**
ARUSHA

MWILI wa Zaituni Jumanne (32), aliyedaiwa kuuawa kwa kunyongwa juzi katika nyumba ya kulala wageni jijini Arusha, ulizikwa jana katika makaburi ya Baniani, Kata ya Unga limited jijini.

Zaituni alikutwa ameuawa akidaiwa kunyongwa na kijana wa kiume katika nyumba ya kulala wageni ya Shivers iliyoko Mtaa wa Kaloleni, wilayani Arusha.

Baba mzazi wa marehemu, Jumanne Ally, Mkazi wa Ngarenaro, akizungumza kwa hisia kali wakati wa maziko, alisema alipokea kwa mshtuko taarifa za kifo cha binti yake wakati akiwa katika shughuli zake za kimaisha.

"Nilipokwenda mochwari ya Hospitali ya Mount Meru, nikajiridhisha ndiye mwanangu aliyefariki dunia. Nikashauriana na kaka yangu na ndugu zangu, tukaamua kumzika na kumwachia Mungu," alisema.

Ally alisema,mwanawe ameacha mtoto anayesoma kidato cha tatu. Ataendelea kumsomesha ili kutimiza ndoto yake.

Alisema kuwa kwa bahati mbaya hajaonana na mtuhumiwa aliyemnyonga mwanawe kutokana na polisi kumzuia kuonana naye kwa kuwa alikuwa na hasira. Baada ya kuzika, alitarajia kwenda polisi kuomba kumwona mtuhumiwa huyo.

Alidai mtuhumiwa wa mauaji hayo anaitwa Christian Macha, mkazi wa Kisongo.

Ilidaiwa na mashuhuda wa tukio hilo juzi kuwa mtuhumiwa wa mauaji hayo alifika katika nyumba hiyo asubuhi na kuchukua chumba, lakini majira ya mchana siku hiyohiyo walishangaa kuona mtuhumiwa anatoka chumbani anakimbia akiwa na nguo ya ndani pekee.

Walidai kitendo hicho kiliwashtua na kuanza kumkimbiza na kumkamata eneo la Mnara wa Mwenge na kumrudisha eneo la tukio ambako kulibainika kufanya mauaji ya Zaituni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha Justine Masejo alisema wataalamu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Mount Meru) wanafanya uchunguzi kubaini chanzo cha kifo hicho ili hatua zaidi zichukuliwe.


ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR

## TAARIFA KWA UMMA

### KUONGEZWA MUDA WA MWISHO WA KULIPA KODI YA MAJENGO

**Zanzibar, 30 Septemba, 2023.**

**1.0 UTANGULIZI:**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), inaufahamisha umma kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2023, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango alitoa Tangazo la Kisheria Nam. 78 la mwaka 2023, (LN.No 78) kuhusu viwango maalum vya kodi ya majengo kwa mwaka 2023/2024 kwa mujibu wa kifungu cha 7A (1) cha Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam.14 ya Mwaka 2008.

Tangazo la Kisheria la kutoza kodi ya majengo kuanzia tarehe 1 Julai, 2023, **LIMESAMEHE KUTOZWA KODI YA MAJENGO kwa MAJENGO YA MAKAAZI yasiyo ya Ghorofa.**

Majengo yafuatayo yatatakiwa kulipa kiasi maalum cha kodi kama ilivyoainishwa katika Jadweli hapa chini:

| SN | AINA YA JENGO | KIASI CHA KODI KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1. | Majengo ya ghorofa ya makaazi au kondominiam | Tzs. 10,000/= kwa kila ghorofa au Jengo (Unit) |
| 2. | Majengo ya biashara yenye ghorofa | Tzs. 50,000/= kwa ghorofa |
| 3. | Majengo mengineyo ya biashara | Tzs. 50,000/= |
| 4. | Majengo ya hoteli:<br>(a) Hoteli ya nyota tano<br>(b) Hoteli ya nyota nne<br>(c) Hoteli ya nyota tatu<br>(d) Hoteli ya nyota mbili<br>(e)Hoteli ya nyota moja<br>(f) Hoteli nyenginezo | Tzs. 500,000/=<br>Tzs. 400,000/=<br>Tzs. 300,000/=<br>Tzs. 200,000/=<br>Tzs. 100,000/=<br>Tzs. 50,000/= |

**2.0 MUDA WA KISHERIA WA KULIPIA KODI YA MAJENGO:**

Kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam. 14 ya Mwaka 2008, kiasi chote cha kodi ya majengo kwa mwaka kinapaswa kulipwa kabla au siku ya tarehe **30,Septemba** ya kila mwaka, na si zaidi ya tarehe **30, Juni** ya mwaka unaofuata.

**3.0 KUONGEZWA MUDA WA MWISHO WA KULIPA KODI YA MAJENGO:**

Kwa mujibu wa kifungu cha Sheria kilichotajwa hapo juu, kodi ya majengo inalipwa kabla au siku ya tarehe 30, Septemba, 2023. Hata hivyo, kutokana na ukweli kwamba, viwango vya kodi ya majengo vimeanzishwa hivi karibuni chini ya alitoa Tangazo la Kisheria Nam. 78 la mwaka 2023, (LN.No 78), hivyo basi hii ni sababu ya msingi na yenye kutosheleza kuongeza muda wa mwisho wa kulipa kodi ya majengo kwa mwaka 2023/2024.

Kwa muktadha huo, na kwa mujibu wa kifungu cha 10 (2) cha Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam. 14 ya 2008, tarehe ya mwisho ya kulipa kodi ya majengo kwa mwaka 2023/2024, imeongezwa kutoka siku ya tarehe ya 30 Septemba, 2023 hadi siku ya tarehe 30 ya Novemba, 2023.

**4.0 MADHARA YA KUTOLIPA KODI YA MAJENGO KWA WAKATI:**

Mmiliki yeyote wa jengo lilolo miongoni mwa majengo yaliyoorodheshwa katika Tangazo la Kisheria Nam. 78 la mwaka 2023, (LN.No 78), anapaswa kulipa kodi ya majengo kabla au siku ya tarehe 30, Novemba,2023, ili kuepuka adhabu kama ilivyotolewa chini ya kifungu cha 33 cha Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Kodi, Na. 7 ya 2009.

**5.0 HITIMISHO:**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar inawataka wamiliki wa majengo husika kutumia vizuri nyongeza ya muda wa mwisho wa kulipa kodi ya majengo katika kutimiza wajibu wao.

Wakati huo huo, ZRA, itaanza kampeni ya uhamasishaji na utaratibu wa ulipaji kodi hii kwa wamiliki wote wa majengo husika ili kuongeza uwajibikaji wa hiari kabla ya tarehe ya mwisho ya kulipa kodi. ZRA inawahakikishia wamiliki wote wa majengo kuendelea kuchukua hatua za kisheria zinazofaa katika kurahisisha ulipaji kodi ya majengo kwa hiari.

**"Tulipe Kodi kwa Maendeleo ya Zanzibar"**

Yusuph Juma Mwenda
**Kamishna Mkuu**

SLP 2072,
SLP 163 (P)

255-24-245255 (
255-24-2233041

www.zanrevenue.org
1 Barabara ya Fumba, 71125 Mjini Magharibi, Zanzibar
262 Barabara ya Chake-Wete, 74206 Wara, Kusini Pemba, Zanzibar (P)

zra@zanrevenue.org

# Waziri ataka TANESCO kuzingatia ratiba ya umeme

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kila linapotaka kukata umeme kwenye maeneo ya uzalishaji, ofisi za umma na watoa huduma wakae na kushauriana nao ili kujua utaratibu sahihi wa kurudisha nishati hiyo.

Aliyasema hayo juzi, jijini Dar es Salaam, baada ya kutembelea kituo cha kuzalisha umeme cha Tegeta kinachozalisha megawati 300.

Alisema maeneo aliyoyataja kama wanafanya shughuli za uzalishaji kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi 12:00 jioni yasikatiwe huduma hiyo kwa muda wote huo.

Pia, Judith aliisisitiza TANESCO kuzingatia ratiba ya kukata na kurudisha umeme, akiitaka kurudishwa kwa wakati, ili watu waendelee na shughuli zao, akieleza kuwa kama watu wamekatiwa umeme asubuhi mpaka saa 12:00 jioni, haitakubalika muda wa kurudisha ukazidishwa.

"Pia nimewaelekeza TANESCO kuhakikisha matengenezo ya mitambo lazima yanafanyika kwa wakati na kwa muda mfupi ili kuendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme na panapotokea hitilafu basi zifanyiwe kazi kwa haraka ili umeme uendelee kupatikana," alisema Judith.

Kadhalika alisema Watanzania wanapopata changamoto za umeme kama hitilafu za Luku, kukatika kwa waya na kuharibika kwa 'transformer' wahakikishe wanazitatua kwa wakati.

"Hatutakubali wananchi walale giza kwasababu transfoma au mita haijarekebishwa kwa wakati, waimarishe mifumo yao waweze kufuatilia wahakikishe wateja wakipata hitilafu wanapata huduma kwa haraka," alisema Judith.

Aidha, wananchi wanapoomba kuunganishiwa umeme katika maeneo yenye miundombinu, waunganishiwe kwa wakati, ili waendelee kufurahia huduma hiyo na kuwa wameweka mifumo ya kisasa ya Nikonekti, ili kupunguza mwingiliano wa kibinadamu na kuondoa mianya ya rushwa.

Alisema changamoto zinapoendelea kutoka kuhusu suala la kuunganisha umeme ni jambo linaloweza kumaliza na kwamba wanaendelea kusimamia na kuhakikisha huduma ya upatikanaji wa nishati hiyo inaendelea kuimarika, kusimamia matengenezo na kufuatilia uzalishaji kwa kiasi kikubwa.

Mkurugenzi wa TANESCO, Gisima Nyamo-hanga, alisema wanafanya kila juhudi zinazowezekana kuwa na umeme wa kutosha kwenye gridi ambao watauga kwa wananchi wautumie katika uendeshaji wa shughuli zao.

"Siku zilizopita tulisema katika gridi kulikuwa na upungufu wa megawati 400 na juhudi tulizokuwa tunaendelea nazo za matengenezo zimesaidia kupunguza upungufu kutoka kiwango hicho hadi 350, lakini kusudio letu mpaka itakapofika mwezi Machi 2024 tuwe tumepunguza tatizo la upungufu.

# Korti Kuu yabariki kifungo cha miaka 30 aliyebaka mwizi wa miwa yake

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Sumbawanga imebariki Okumu Raurence kutumika kifungo cha miaka 30 gerezani kwa kosa la kubaka mwanafunzi wa miaka 13, akidai kaiba miwa yake.

Hukumu ya mahakama hiyo ilitolewa juzi, ikiridhia pia mrufani apewe adhabu ya viboko 12 na kumlipa mwathirika fidia ya Sh. milioni moja.

Mahakama hiyo, mbele ya Jaji Thadea Mwenempazi, ilitoa uamuzi huo baada ya kutupilia mbali rufani iliyokatwa na Raurence, akipinga hatia na adhabu aliyopewa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Katavi.

"Ushahidi wa upande wa mashtaka ulikuwa wa nguvu na umeweza kuthibitisha mashtaka dhidi ya mrufani kulinganisha na ushahidi wa utetezi.

"Mwathirika alieleza vyema mahakamani jinsi alivyoingia mikononi mwa mrufani alipokwenda kuokota matunda akiwa na rafiki yake anaitwa Leah," alisema Jaji Thadea.

Ilidaiwa mahakamani kuwa Juni 21, 2021, mwathirika alikwenda shuleni, saa tatu asubuhi akiwa na rafiki yake, walikwenda kuchukua matunda jirani na eneo la shule.

Mrufani alitokea katika eneo hilo. Rafiki wa mwathirika alikimbia, lakini mwathirika hakukimbia kwa kuwa alichelewa kumwona.

Mrufani alimkamata na kumwambia kwamba alishakamata wanafunzi wengine wanaiba miwa. Aliomba amsamehe, lakini alikataa, akataka afanye naye mapenzi. Mwathirika aliomba apewe adhabu nyingine, lakini mrufani alikataa. Alimvua nguo, akamlazimisha alale chini kisha akambaka.

Ilidaiwa mwanafunzi huyo alikwenda kutoa taarifa kwa mwalimu mkuu ambaye alitoa taarifa kwa Ofisa Mtendani, naye akatoa taarifa kwa Jeshi la Polisi na kufanikisha kukamatwa kwa mrufani.

Mahakama ilieleza kuwa ushahidi wa mrufani umeungwa mkono na ushahidi wa kitabibu ambao ulithibitisha kubakwa kwa mwathirika pamoja na kujeruhiwa.

Kutokana na maelezo ya pande zote mbili, mahakama iliona hoja za rufani hazina mashiko na hivyo ikaitupilia mbali kama ilivyoombwa na upande wa wajibu rufani.

Katika rufani hiyo, mrufani alikuwa na hoja mbili ikiwamo ya mahakama ya chini ilikosea kumtia hatiani na kumhukumu ikiwa mrufani hakuweza kutambuliwa vyema na mwathirika.

Hoja nyingine ni kwamba mahakama ya chini ilikosea kumhukumu kwa kuzingatia utetezi wake dhaifu badala ya kuangalia uthibitishwaji wa kesi bila kuacha shaka.

Mrufani alidaiwa kutenda kosa hilo Juni 21, 2021 katika Kijiji cha Kasekese, Wilaya ya Tanganyika, Mkoa wa Katavi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
04.10.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kati ya tarehe **12-10-2023** hadi **15-10-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es- Salaam Port** kuelekea **Rufiji,** gari hizo zina namba za usajili: **T 295 EDD / T 387 DHQ T 289 EDD / T 394 DVS T 180 DFC / T 416 AYQ T 896 DSD / T 310 DDH T 973 DTN / T 879 EAU T 308 EDD / T 393 DVS T 914 DSD / T 568 EAZ**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 7.20**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: ***Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti,*** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
04.10.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kati ya tarehe **12-10-2023** hadi **15.10.2023** kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es- Salaam Port** kuelekea **JNHPP SITE,** gari hizo zina namba za usajili: **T 249 EAZ / T 499 DZX T 203 DYJ / T 777 AQR T 453 DYG / T 881 EAU T 167 DFC / T 390 DHQ T 911 DSD / T 877 EAU T 628 DFA / T 321 DDH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 7.20**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM** hadi **JNHPP SITE** kupitia **KILWA ROAD,** KIBITI, MLOKA. Gari zitasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 06:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka **Dar es Salaam Port** mpaka **Bungu.** Kutoka Bungu kwenda JNHPP Site gari zitasafiri muda wa mchana ***( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


# Jaji Mkuu aweka wazi kigezo kupima utendaji majaji wapya

**Na Mwandishi Wetu,** LUSHOTO

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma amewaambia majaji wapya wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu kuwa ufanisi na utendaji wao wa kazi utapimwa kwa jinsi watakavyoshughulikia majalada ya mashauri mahakamani mara tu baada ya kuanza kazi hiyo.

Prof. Juma alitoa kauli hiyo juzi alipofungua mafunzo elekezi kwa majaji wapya wanne wa Mahakama ya Rufani na 20 wa Mahakama Kuu yanayofanyika katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), wilayani Lushoto mkoani Tanga.

Mafunzo hayo ambayo kwa majaji wa Mahakama ya Rufani yatachukua wiki moja na wiki tatu kwa majaji wa Mahakama Kuu, yameandaliwa na Mahakama ya Tanzania na kuendeshwa na IJA.

"Uwezo wako katika utoaji huduma utapimwa kila siku utakapoingia mahakamani, na kwa kila jalada na utakalolisimamia na kila utakalofanya na kusema litapimwa. Viongozi wako watakupima, wananchi na wadau watakaofika mbele yako watakupima na kutoa tathmini juu ya utendaji wako," alisema Jaji Mkuu.

Prof. Juma aliwataka majaji hao kuishi maisha ya kawaida na kutotumia nafasi zao kwa manufaa binafsi. Aliwakumbusha kuwa tayari kutoa huduma kwa njia ya kidigitali. Mhimili wa Mahakama hautarudi nyuma kwenye matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Washiriki wa mafunzo hayo watapitishwa katika mada mbalimbali ambazo zitawasilishwa na wawezeshaji kutoka Mahakama ya Tanzania na taasisi mbalimbali za umma na binafsi.

Jaji Kiongozi, Mustapher Siyani, wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo aliwaambia majaji hao kuwa mahakama na wananchi wana matarajio makubwa kwao, hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa ufanisi na kasi kubwa mara tu baada ya kumaliza mafunzo yao.

"Tuna matarajio makubwa kuwa mara baada ya kupatiwa mafunzo haya, mtashuka kwenye vituo mlivyopangiwa mkiwa mnakimbia kama askari mpya, mfahamu sisi sote na Watanzania kwa ujumla tunasubiri kwa hamu kubwa utendaji kazi wenu," alisema Jaji Siyani.

Mkuu wa IJA ambaye pia ni Jaji wa Mahakama ya Rufani, Paul F. Kihwelo alisema mafunzo hayo yameandaliwa ili kuwajenga majaji hao katika kazi yao mpya ya ujaji. Mada zimeandaliwa ili kukidhi kiu ya washiriki.

Majaji hao wapya waliteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan Septemba 3 mwaka huu na kuapishwa Septemba 14 mwaka huu Ikulu jijini Dar es Salaam.

Kuteuliwa na kuapishwa kwa majaji hao wapya kunaongeza idadi ya majaji wa Mahakama ya Rufani kufikia 30 na wa Mahakama ya Kuu kuwa 105.

Ufunguzi wa mafunzo hayo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo majaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel, wasajili wa ngazi mbalimbali za Mahakama ya Tanzania na viongozi kutoka taasisi mbalimbali za umma.

Mafunzo hayo elekezi ya awali ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Mafunzo ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2013, Mpango Mkakati wa Mahakama ya Tanzania 2021/22-2024/25, Sera ya Mafunzo ya Mahakama ya Tanzania ya Mwaka 2019 na Mpango Mkakati wa IJA wa Mwaka 2023/24-2027/28.

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU MAKUSANYO YA KODI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA YA MWAKA WA FEDHA 2023/24 (JULAI HADI SEPTEMBA, 2023)

**Dar es Salaam, 03 Oktoba, 2023:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuufahamisha umma kuwa katika kipindi cha robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2023/24 (**mwezi Julai hadi Septemba**) imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Trilioni 6.58**, sawa na ufanisi wa **asilimia 97.53** ya lengo la kukusanya **Shilingi Trilioni 6.75**. Makusanyo haya ni sawa na ongezeko la **asilimia 11.05** ikilinganishwa na makusanyo ya **Shilingi Trilioni 5.92** yaliyofikiwa katika kipindi kama hiki katika Mwaka wa Fedha 2022/23.

Katika kipindi cha mwezi **Septemba 2023**, TRA imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Trilioni 2.63**, ikiwa ni ufanisi wa **asilimia 108.41** ya lengo la kukusanya kiasi cha **Shilingi Trilioni 2.42**. Makusanyo haya ni ongezeko la **asilimia 15.49** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi Trilioni 2.27** kilichokusanywa katika mwezi kama huu katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Takwimu za makusanyo kwa kila mwezi katika kipindi tajwa zinaoneshwa katika **Jedwali Namba 1**.

**Jedwali Na.1: Makusanyo ya Mapato kwa Kipindi cha Julai hadi Septemba 2023/24 (Shilingi Milioni)**

| Mwezi | 2022/23 | 2023/24 | | | Ukuaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | Makusanyo | Lengo | Makusanyo | Ufanisi | |
| Julai | 1,764,365.23 | 2,142,898.37 | 1,939,021.30 | 90.49% | 9.90% |
| Agosti | 1,886,416.55 | 2,180,132.27 | 2,014,060.83 | 92.38% | 6.77% |
| Septemba | 2,273,711.23 | 2,422,262.71 | 2,625,923.50 | 108.41% | 15.49% |
| **Jumla** | **5,924,493.01** | **6,745,293.35** | **6,579,005.63** | **97.53%** | **11.05%** |

***Chanzo:*** *Mamlaka ya Mapato Tanzania*

Mafanikio haya yaliyofikiwa katika robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2023/24 ni matokeo ya hatua mbalimbali zikiwemo: -

i). Maelekezo na miongozo mbalimbali inayotolewa na **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** pamoja na viongozi wengine wa Serikali katika ngazi mbalimbali;

ii). Kuongezeka kwa **uwekezaji na ukuaji wa shughuli za kiuchumi** hapa nchini kama vile uzalishaji viwandani, uingizaji wa bidhaa nchini na kuimarika kwa shughuli za utalii;

iii). Kuongezeka kwa matumizi ya **mifumo ya TEHAMA** katika shughuli za usimamizi wa kodi na hivyo kurahisisha utoaji wa huduma na kukuza uhiari wa kulipa kodi;

iv). Kuongezeka kwa **ufahamu na hamasa** kwa wananchi kuhusu masuala ya kodi kupitia kampeni mbalimbali kama vile ***Mlango kwa Mlango*** na ***Tuwajibike*** zinazoendelea katika mikoa yote nchini.

TRA inapenda kutoa shukrani za dhati kwa walipakodi wote walioonesha **uzalendo** wa hali ya juu kwa nchi yetu kwa njia ya ulipaji wa kodi kwa hiari katika kipindi cha robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2023/24. Pia, tunapenda kuwahakikishia walipakodi wote na umma kwa ujumla kuwa tumejipanga vema katika kuboresha usimamizi wa kodi nchini ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa walipakodi kwa kuongeza usajili, kuboresha kiwango cha utoaji huduma, kuongeza utoaji elimu ya kodi, kuboresha mahusiano na walipakodi na kuongeza kiwango cha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji huduma.

Mwisho, TRA inapenda kuwakumbusha walipakodi wote nchini kuendelea kuzingatia matakwa mbalimbali ya sheria za kodi ikiwemo **kutoa risiti za kielektroniki (EFD Receipts) kwa kila mauzo, kuwasilisha ritani za kodi na kulipa kodi stahiki kwa wakati.**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

A. J . Kidata
**Kamishna Mkuu**

217626702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha maofisa ugani kisikike

**MOJA** ya kipimo cha mfanyakazi kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi ni pamoja na kuwa na vitendea kazi vitakavyomrahisishia kufikia lengo lake.

Lakini vitendea kazi hivyo ni lazima viwe na nyenzo zitakazoviwezesha kufanya kazi yake.

Kuna hiki kilio cha maofisa kilimo wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, kupatiwa pikipiki kuwawezesha kuwafikia wakulima kwa urahisi, lakini wakidai kuwa hawajapatiwa mafuta kama ulivyo utaratibu hali inayowafanya kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Imeelezwa kuwa wanatakiwa kuwekewa mafuta kwenye pikipiki zao kupitia Mfuko wa Halmashauri kuwawezesha kuwafikia wakulima shambani na kuwapatia elimu ya kulima kisasa mazao ya chakula, biashara, lakini kukosekana kwa mafuta hayo kunasababisha wakulima kukosa elimu kulima kisasa.

Kilimo ni uti wa mgongo, nchi inategemea kilimo kwa mazao ya chakula na biashara kuiwezesha kuwalisha wananchi wake na kupata pesa kupitia watakaouza nje kibiashara.

Kilimo bora ni kile ambacho wakulima watapata elimu itakayowasaidia kujua mbegu zipi zinastawi sehemu husika ili kupata mazao bora na mengi na kupata ziada ya chakula. Vilevile, umuhimu wa kupima udongo ili kubaini kama unarutuba ya kuzalisha mbegu zinazokusudiwa kupandwa.

Kwa mujibu wa Ofisa Kilimo Kata ya Kinamapula Halmashauri ya Ushetu, Fadhili Kadyue, wanashidwa kutekeleza majukumu yao kutokana na kutokupewa mafuta kwa ajili ya pikipiki walizopewa.

Wamewapatia vyombo hivyo vya usafiri, lakini hawajawapatia fedha za matengenezo na mafuta ya kuwawezesha kuwafikia wakulima hali inayoathiri mzunguko wa kuwafikia kwa wingi wakulima wote na kuwaelimisha kulima kisasa kulingana na maeneo yao ya kilimo.

Kutokana na kukosa nishati hiyo kwenye vyombo vya usafiri waliopewa, inawabidi kutumia mikutano ya hadhara inayoitishwa na diwani, mihadhara ya kidini na vikundi vya kuweka na kukopa vilivyopo kwenye kata na kutoa elimu ya kulima kisasa.

Kwa mujibu wa Ofisa Kilimo huyo, kata yake ina vijiji sita ambavyo ni Kinamapula, Kalama, Ilevye, Hongwa, Butibu na Kasomela na kwa wiki anahakikisha anavitembelea vyote kulingana na mafuta atakayokuwa nayo baada ya kupatikana kwa mshahara wake na kuiomba serikali kuliangalia suala hilo ili wawafikie zaidi wakulima kusaidia mavuno kupatikana kwa wingi.

Wakulima kwa upande wao wanalalamikia maofisa hao kutofika kwenye maeneo yao ipasavyo kwa kile wanachoeleza kuwa ni ukosefu wa mafuta.

Wakulima wengi wanalima kienyeji kutokana na kutokufikiwa kwa wakati.

Baadhi ya maofisa kilimo wanatumia fedha zao binafsi kujaza mafuta katika pikipiki hizo kitendo kinachowafanya kupunguza ufanisi wa kazi za kuwatembelea wakulima, kuwafikia wachache kati ya wengi.

Pamoja na malalamiko ya maofisa ugani hao, Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Ushetu alikiri kutowapatia mafuta na matengenezo ya pikipiki maofisa ugani wake na kuwataka kuwa waaminifu pindi wanaponunua mafuta kwa fedha zao binafsi wakati utaratibu wa fedha hizo ukiendelea kuwekwa sawa.

Kiutaratibu wanapaswa kupewa mafuta kila mwezi si chini ya lita mbili na matengenezo ya pikipiki.

Maofisa ugani wasikate tamaa ya kazi kwa ukosefu wa mafuta utaratibu ukishawekwa sawa mambo yatakuwa vizuri. Wahudumieni wakulima wazalishe mazao bora na mengi kwa elimu mtakayowapa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Rushwa ngono inaandaa vihio



Na Reubeni Lumbagala

**RAIA** wakipata elimu bora, ni rahisi kujipatia maendeleo iwe kisiasa, kijamii na kiuchumi, lakini ili taifa liwe na wasomi bora lazima kuwe na viwango.

Wanafunzi wa ngazi zote waandaliwe kupata maarifa, ujuzi na stadi stahiki zinazohitajika ili kumudu fani watakazotumikia katika taasisi mbalimbali.

Kutokana na unyeti wa sekta ya elimu katika kuandaa raia walioelimika na wenye maarifa ya kutosha ili watumikie taifa lao, kuzingatia maadili ili kupata wasomi bora kwa maendeleo hakukwepeki.

Hivyo walimu, wakufunzi na wahadhiri waliopewa dhamana ya kufundisha wanafunzi lazima muwe na maadili na mzingatie miiko ya kazi zenu ili kutimiza azma ya serikali ya kuandaa wasomi wenye viwango vya ushindani kitaifa na kimataifa.

Lakini, kinachokera zama hizi ni kukithiri rushwa ya ngono katika taasisi za elimu kuanzia msingi hadi vyuo vikuu.

Rushwa hiyo ni adui anayekwamisha kupatikana wasomi bora wenye weledi na sifa stahiki wanaohitajika katika jamii, mashirika, taasisi na ofisi za umma na hata nje ya mipaka kutoa mchango wa kimaarifa na kiuzoefu kufikia maendeleo.

Ni ukweli ulio dhahiri kuwa palipo na rushwa ya ngono, kupata wasomi, viongozi na watumishi vihio hakukwepeki, kwani hawatakuwa na uwezo.

Katika dunia ya sasa yenye ushindani na maarifa mengi, wasomi au wahusika wanaopatikana kupitia rushwa hawana nafasi. Changamoto ya rushwa ya ngono katika vyuo vya kati na vyuo vikuu, kwa mujibu wa Ripoti ya TAKUKURU, Mkoa wa Kinondoni inayowasilishwa na Mchunguzi Mkuu na Mwendesha Mashtaka wake, Bibie Msumi inaonyesha asilimia 60 ya watuhumiwa na rushwa ya ngono ni wahadhiri wa vyuo hivyo.

Bibie anayasema hayo kwenye kikao cha majadiliano kilichoandaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), kikishirikiana na Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T) kwenye mradi wa kuangazia rushwa ya ngono kwa waandishi wanawake.

> **Lakini, kinachokera zama hizi ni kukithiri rushwa ya ngono katika taasisi za elimu kuanzia msingi hadi vyuo vikuu**

Kwa mujibu wa utafiti wa 2020 unaofanywa na TAKUKURU watuhumiwa wengi waliokamatwa kwa makosa ni wahadhiri wa vyuo vikuu na vya kati na kwamba baadhi yao hukumu zimeshatolewa na wengine kesi zinaendelea mahakamani.

Vyuo vikuu na vya kati ni taasisi zinazotegemewa kuandaa na kuzalisha wasomi bora kwa ustawi na maendeleo ya taifa, uwepo wa rushwa ya ngono vyuoni humo una hatarisha mustakabali wa kupatikana wataalamu wa afya, kilimo, wahandisi, walimu na viongozi bora.

Rushwa hiyo isipodhibitiwa, kuna hatari ya kutumia gharama kubwa zikiwamo za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) kuzalisha wasomi mambumbumbu watakaokuwa na ufaulu wa alama za juu (GPA) lakini vichwani hawana kitu.

Mathalani, mwanafunzi wa shahada ya kwanza aliyetoa rushwa ngono akapata ufaulu mkubwa anaweza akapata ufadhili wa chuo kuendelea na shahada ya uzamili ili awe mhadhiri msaidizi, chuoni kwake.

Lakini, kwa vile ni mbumbumbu mhitimu wa aina hiyo hatakuwa mahiri kwani hajui kitu na ufaulu wake ni zao la rushwa ngono na si maarifa, akili wala juhudi.

Vilevile, wahitimu wa kozi za afya, kilimo, uhandisi, uhasibu na nyinginezo watashindwa kumudu majukumu yao ya kazi endapo watakuwa ni zao la rushwa ngono walipokuwa vyuoni.

Uwekezaji mkubwa unaofanywa kwenye elimu kuanzia uboreshaji wa miundombinu, walimu mikopo, hautatoa matokeo chanya kama rushwa ngono itaendelea.

Jamii kwa pamoja tunapaswa kuipinga kwani ni adui wa juhudi za mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia umaskini na maradhi katika nchi hii.

Katika vita hii, wanawake wanategemewa sana katika kuwafichua wahusika kwani ndiyo wahanga wakubwa, kuendelea kunyamazia vitendo hivi, ni kuunga mkono rushwa ngono na kuhujumu juhudi za serikali za kuinua sekta ya elimu.

## Watanzania, raia wa India wakumbushwa kuwaenzi Nyerere, Gandhi

**Na Romana Mallya**

WATANZANIA na raia wa India wamekumbushwa kuleta maendeleo chanya ndani ya nchi hizo, kwa kuwaenzi kwa vitendo na kufuata mafundisho ya waasisi wa mataifa hayo, Mwalimu Julius Nyerere na Mahatma Gandhi.

Wamekumbushwa kuwa waasisi hao waliamini katika elimu kuwa ni njia muhimu ya kufanya nchi hizo kuendelea.

Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan, aliyasema hayo juzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 154 tangu kuzaliwa kwa muasisi wa Taifa la India, Mahatma Gandhi.

Maadhimisho hayo yalikwenda sambamba na siku ya kupinga vurugu duniani ambayo yalihudhuriwa na watu mbalimbali wakiwamo Diaspora wa India na wanafunzi.

Balozi Binaya alisisitiza kuwa waasisi hao walikuwa na mitazamo inayofanana kuhusu kupambania uhuru wa nchi zao na kupinga vurugu.

Alisema wote waliamini katika elimu kama njia muhimu ya kufanya nchi hizo kuendelea.

"Misingi waliyoisimamia bado inaendana na mazingira ya sasa, hivyo ni vyema Watanzania na raia wa India tukaitumia kama njia ya kuenzi mambo mazuri na mema waliyoanzisha waasisi hawa," alisisitiza.

Alisema wanatumia siku hiyo kukumbuka misingi ya Baba wa Taifa la India aliyosimamia na mchango wa Bara la Afrika katika uhuru wa India.

Alikumbusha kuwa, Gandhi aliishi Afrika kwa muda mrefu na aliporudi India ndipo nchi hiyo ilipompata mpigania uhuru.

"Tunaitumia siku ya leo katika kukumbuka misingi aliyoisimamia Gandhi na mchango wa bara la Afrika katika uhuru wa India, ambapo aliishi Afrika kwa muda mrefu na aliporudi India ndipo tulipata mpigania uhuru," alisema.

Mkuu wa Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Hezron Kangalawe, aliupongeza Ubalozi wa India nchini kwa kuandaa tukio hilo ambalo ni muhimu katika kuwakumbuka waasisi hao walioyapa heshima mataifa yao.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni wa India, Swami Vivekaranda (SVCC), Dk. Soumya Chavan, alisema Gandhi alikuwa kiongozi mkubwa na mpiganiaji wa uhuru aliyezaliwa Oktoba 2, 1869 huko Gujarat.

"Alianza harakati mbalimbali nchini India kama sehemu ya mapambano ya uhuru, anajulikana kwa kanuni zake za kutokuwa na vurugu, mkweli na mwaminifu," alisema.






Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba (katikati), akikata utepe kuzindua kituo kipya cha mafuta cha kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, eneo la Kinyerezi Tabata, Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja. Kulia kwake ni Diwani wa Kata ya Kinyerezi, Leah Mgitu, (kushoto kwake) ni Mkurugenzi Mkuu mpya wa Kampuni hiyo, Mamadou Ngom na Mkuu wa Kitengo cha Sheria, Masuala ya Mashirika, Rasilimali Watu na Utawala, Getrude Mpangile. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chongolo awataka wajawazito kujifungulia vituo vya afya

**Na Neema Hussein,** TANGANYIKA

KATIBU Mkuu CCM Taifa, Daniel Chongolo, amewataka wajawazito kujifungulia vituo vya afya ili kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Alisema hayo alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Ikola katika Wilaya ya Tanganyika, mkoani Katavi, baada ya kutembelea na kukagua kituo cha afya Ikola kilichojengwa kupitia fedha za mapato ya ndani na nguvu za wananchi.



Alisema takwimu zinaonyesha vifo vingi vya wajawazito katika Wilaya ya Tanganyika vinatokana na kinamama kujifungulia majumbani.

"Lengo la serikali kusogeza huduma hizi ni kumlinda mama, tunapata vifo vya mama na mtoto ambavyo vinaepukika na vingi vinatokana na kinamama kujifungua kwa njia ya kienyeji, achaneni na mila hizo nendeni kwenye vituo vya afya na hospitali zetu," alisema Chongolo.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa kituo hicho, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Alex Mrema alisema kimegharimu Sh. milioni 408, milioni 400 ni mapato ya ndani, na milioni nane zimetokana na nguvu za wananchi.

"Mradi huu ulianzishwa ili kukidhi mahitaji ya watu wa Ikola na vijiji jirani kutokana na kutokea mara kwa mara kwa magonjwa ya milipuko, mradi huu unasaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto, kupunguza gharama wanazoingia wananchi kwenye kutibiwa Hospitali ya Rufani Manispaa ya Mpanda," alisema Dk. Mrema.

**Alisema takwimu zinaonyesha vifo vingi vya wajawazito katika Wilaya ya Tanganyika vinatokana na kinamama kujifungulia majumbani.**

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, alisema wakisubiri mapato ya ndani ya halmashauri ya kila mwaka itachukua muda mrefu kukamilisha mchakato wa kukifanya kituo hicho kuwa hospitali teule ya wilaya kwa upande wa Ikola na kuiomba serikali wapate usaidizi wa fedha kutoka serikali kuu.

Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, Seleman Kakoso, aliiomba serikali kuongeza idadi ya watumishi wa afya katika vituo vya afya katika wilaya hiyo ili huduma iendane na uzuri wa majengo yaliyopo na wingi wa hospitali hizo.

Wananchi wa eneo hilo wameishukuru serikali kwa kufanikisha ujenzi wa kituo hicho na kufanya waondokane na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Hakimu ataja sababu washtakiwa kesi za ukatili kuachiwa huru

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

USHAHIDI hafifu pamoja na kasoro mbalimbali wakati wa upelelezi wa kesi za matukio ya ukatili, ikiwamo ya ubakaji vimetajwa kuwa sababu zinazochangia washtakiwa wa matukio hayo kuachiwa huru.

Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Geita, Johari Kijuwile, aliyasema hayo wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wa idara zinazohusika na ulinzi wa mtoto na masuala ya kupinga ukatili yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Plan International kupitia mradi wa Kagis, unaolenga kuhakikisha mtoto wa kike anabaki shuleni.

Alisema kesi nyingi mtenda kosa huachiwa huru kutokana na upelelezi kutofanyika kwa kina na upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha pasi na shaka.

"Mara nyingi upande wa upelelezi una acha watu muhimu kwenye ushahidi mfano mtoto amebakwa haletwi mahakamani kutoa ushahidi wanamalizа kifamilia kesi italetwa mahakamani itatajwa, lakini mwisho wa siku itatupiliwa mbali na jamii itaona haki haitendeki," alisema Kijuwile.

Msimamizi wa Masuala ya jinsia kutoka Shirika la Plan International linalotekeleza mradi wa kuwawezesha wasichana wa rika balehe kuendelea na masomo (Kagis), Hildegada Mashauri, alisema miongoni mwa sababu zinazokwamisha ushahidi ni uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya ukatili pamoja na kutojua hatua za kufuata mtu anapofanyiwa ukatili.

Alisema kutokujua hatua za kufuata sio tu kunamnyima mwathirika wa ukatili haki kwenye vyombo vya sheria, bali pia inaweza kusababisha maambukizi ya virusi vya Ukimwi kama hatapata huduma ndani ya saa 72.

"Tumewakutanisha wataalam ambao ni watendaji, walimu, maafisa maendeleo ya jamii, maafisa ustawi wa jamii, mahakimu na watu wa dawati la jinsia ili watambue njia sahihi ambazo mhanga akishatoa taarifa aliyepewa anapaswa aipeleke kwa nani na kwa wakati gani," alisema Mashauri.

Alisema, mradi huo unaofadhiliwa na serikali ya watu wa Cananda katika mkoa wa Kigoma na Geita umewakutanisha wataalamu hao lengo likiwa ni kuhakikisha jamii hasa wasichana wanapata ulinzi na usalama na kuishi kwenye mazingira huru ambayo hayana ukatili wa kijinsia.

Mkuu wa dawati la jinsia na watoto mkoa wa Katavi, Judith Mbukwa akizungumza kwenye mafunzo hayo alisema wazazi au walezi kutowajibika katika malezi na makuzi ya watoto husababisha mmomonyoko wa maadili na kuchangia kuwapo matukio ya ukatili.

Ofisa Mtendaji Kata ya Nyamigota, Kazmiri Pascal, alisema uelewa mdogo wa masuala ya ukatili umechangia jamii kuona ni jambo la kawaida kumpiga mke au mtoto na ili kuukomesha elimu bado inahitajika ili jamii iweze kuachana na mila na desturi zinazo mkandamiza mtoto au mwanamke.

Taarifa za Jeshi la Polisi nchini za mwaka 2022 zinaonyesha matukio ya ukatili kwa watoto yalikuwa 12,163 na kati yao 9,962 ni watoto wa kike.

Takwimu hizo zinaonesha matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoongoza ni pamoja na ubakaji 6,335; Kulawiti 1,555 mimba za utotoni 1,557 kuzorotesha masomo 808 na mashambulizi yalikua 231.



Mkurugenzi Mkuu, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, akizindua maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja 2023. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NSSF yajivunia kuthamini, kuheshimu wateja wake

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umezindua maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja 2023 katika hafla iliyofanyika Ofisi za Mfuko, Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo wenye kaulimbiu Team Service' Mkurugenzi Mkuu, Masha Mshomba, alisema NSSF inaendelea kuthamini, kutambua na kuheshimu michango ya wateja wake kwa kutoa huduma bora kupitia watumishi wenye uweledi na ari ya kufanya kazi.

Pia, kaulimbiu ya Mfuko ni 'Ushirikiano kwa Huduma Bora'.

Mshomba alisema mafanikio ya NSSF yamechangiwa na kuwapo wanachama na wanaendelea kuthamini uwapo wao, huku akisisitiza kuwa uongozi madhubuti wa serikali umechangia mafanikio ya Mfuko.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan baada ya kuingia madarakani anaendelea kuhakikisha kuwa serikali yake inaboresha maisha ya Watanzania kwa kutoa huduma mbalimbali zikiwemo za afya, elimu, miundombinu pamoja na huduma nyingine za kijamii ambazo zinaenda kuimarisha uchumi wa taifa na wananchi mmoja mmoja," alisema. Pia, alisema mifuko ya hifadhi ya jamii imefarijika kutokana na kazi kubwa inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, hasa kuhakikisha inaendelea kufanya vizuri, inakuwa na stahamilivu na inafanya majukumu yake ya msingi ikiwamo kulipa mafao mbalimbali ndani ya muda uliowekwa kisheria.

"Tunamshukuru sana Rais Dk. Samia kwa kuleta ustahamilivu katika sekta ya hifadhi ya jamii na tunamuomba aendelee kutusimamia na kuhakikisha mifuko hii siku zote inatimiza malengo yake makuu," alisema Mshomba.

Kadhalika, alisema Mfuko unatambua malengo ya wateja wake na ameahidi kutoa ushirikiano ili nao waweze kuendelea kutoa michango yao.

Alipongeza kazi kubwa inayoendelea kufanywa na Ofisi ya NSSF Kinondoni kutokana na katika kipindi kifupi tokea kuanzishwa kwake imeweza kupata mafanikio makubwa hasa katika yale majukumu ya msingi kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kulipa mafao mbalimbali.

Naye, Meneja wa NSSF Mkoa wa Kinondoni, Large Materu, amesema katika kipindi cha robo ya mwaka tokea ilipoanzishwa ofisi hiyo, imefikia malengo yake kwa asilimia 86 huku makusanyo wakifikia zaidi ya asilimia 90, ulipaji wa mafao mbalimbali wamefikia asilimia 90.37 na katika sekta isiyo rasmi wameshavuka lengo walilowekewa kwa kuandsikisha wanachama wengi zaidi.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, alimshukuru Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, ambaye ameendelea kuwafanya wafanyakazi wote wa Mfuko kuwa wamoja na kufanyakazi kwa ushirikiano na upendo huku pia akipongeza mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa na Ofisi ya Kinondioni ndani ya muda mfupi.

Rehema Chuma, Meneja wa Sekta isiyo rasmi, amesema Serikali kupitia NSSF imejipanga kuwafikia Watanzania wengi waliopo katika sekta isiyo rasmi kunufaika na hifadhi ya jamii kwa kujiunga na kuchangia NSSF ambapo kwa sasa Mfuko unaendelea kukamilisha taratibu ili kuzindua rasmi Mpango wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta isiyo Rasmi ambao utawavutia wananchi wengi.

## Wanafunzi wabuni mfumo kupata nyumba bila dalali

**Na Christina Mwakangale**

WANAFUNZI watano wa Shule ya Sekondari Wailesi, Wilaya ya Temeke, mkoani Dar es Salaam, wamebuni mfumo wa kumwezesha mpangaji kupata nyumba ya kupanga kupitia mtandao, kumrahisishia mpangaji, kuepukana na mkono wa madalali.

Naomi John na wenzake, Yusra Anuary, Restuta Raphael, Joseph Mrope na Vanessa Bethiman, wamesimulia walivyokuja na mbinu hiyo ili kuwaondolea adha wapangaji itokayo kwa madalali, ambao vigezo vya kupatikana nyumba ni ujira wa kodi ya mwezi mmoja.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, wakati wa uwasilishaji wa mradi wao, Naomi alisema upo chini ya mpango wa 'Skills for their Future' ukifadhiliwa na Shirika la Brac, dhumuni ni kusaidia jamii kuondokana na changamoto ikiwamo upatikanaji wa makazi hususan katika miji mikubwa.

"Tulikuwa na mbinu hii baada ya kugundua mwenye nyumba na mpangaji wote wanahitajiana, ila hawakutani. Mfumo huu ni rahisi mtandaoni ukijaza maswali machache utakupeleka kuliko na nyumba, kisha mpangaji, mwenye nyumba watamalizana bila kuwapo mtu wa kati (dalali)," alisema Naomi.

Ofisa Elimu Manispaa ya Temeke, Dk. Janeth Barongo, mgeni rasmi katika tukio hilo, lililofanyika mwishoni mwa wiki, mkoani hapa, aliwapongeza vijana hao ambao wanaunga mkono na msisitizo uliopo kwenye sekta ya elimu kujikita kwenye mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

"TEHAMA ndio msingi ili kuisukuma sekta hii ambayo ina mahitaji makubwa kwenye jamii, shule ya sekondari Wailesi, Karibuni na Mibulani zilizopo manispaa hii ni mfano bora. Aplikesheni zilizoundwa na wanafunzi hawa zitumiwe vyema na jamii kupitia mitandao, kupunguza changamoto zilizopo kwenye sekta hiyo," alisisitiza.

Aidha, wanafunzi wa shule zingine walionesha ubunifu wao mtandaoni ikiwamo namna ya kuweka miadi na daktari hospitalini na wa kutunza notisi za masomo ya darasani.

Meneja Mradi wa 'Skills for their Future' kutoka Brac Maendeleo, Upendo Daudi, alisema mradi unalenga kuwawezesha wanafunzi kubuni na kupata ujuzi, kwa ajili ya baadaye.

"Mradi unajumla ya wanafunzi 640. Wanafunzi wa shule ya sekondari Karibuni na Wailes zilizoko Temeke, zikijumuisha wanafunzi 200. Shule ya Sekondari Miburani wanatoka wanafunzi 240 wanaojifunza masomo ya TEHAMA, ili iweze kuwasidia," alisema Upendo.



## Wanakijiji wajengewa shule kuwaepusha wanafunzi na umbali

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WAKAZI wa Kijiji cha Mvungwe Kata ya Songe, Wilaya ya Kilindi wamefurahia mpango wa serikali wa kujenga shule ya sekondari kijijini hapo ili kuwaondolea wanafunzi adha ya kutembea umbali wa kilometa 16 kila siku.

Wakielezea mradi huo, wananchi hao walidai licha ya kuwa ni mkombozi kwa watoto wao lakini pia utasaidia kupandisha ufaulu wa watoto sambamba na kupunguza utoro shuleni.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi hao, Omar Mabundu alisema ujenzi wa sekondari hiyo imeleta neema kubwa kwao kwa sababu hivi sasa watoto wanalazimika kwenda kufuata elimu katika Shule ya Seuta.

"Sisi wazazi tumelipokea kwa furaha sana jambo hili, mateso ya watoto wetu ni makubwa kwani hivi sasa kila siku hutembea kilometa 16 kwenda na kurudi inatupa shida sana kitaalamu endapo mwanafunzi anaweza kuwa na afya ya mwili na kumsikiliza mwalimu darasani" alifafanua Mabundu.

Naye Bakari Mussa alisema wakazi wa kijiji hicho chenye vitongoji nane wameupokea kwa mikono miwili mradi huo, huku akiahidi yeye na wakazi wenzake kutoa ushirikiano wa hali na mali katika kujenga shule hiyo.

Akizungmza na wananchi katika mkutano wa hadhara wa kijiji hicho, Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Ramadhan Dhahabu alieleza kuwa huo ni mpango wa serikali wa kuwasogezea karibu huduma muhimu wananchi.

Aidha, alitangaza utaratibu kwa wananchi na viongozi wa vijiji kwamba inapotokea jambo linalohusu wakulima na wafugaji itumike busara katika kushughulikia na kuhakikisha ridhaa inapatikana kwa kila upande bila upendeleo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mvungwe, Juma Lupatu na Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Mariam Mpuluzi walieleza namna walivyojiandaa kuupokea mradi huo ikiwemo kutenga eneo la ujenzi, kuandaa miundombinu ya barabara sambamba na kutoa hamasa kwa wananchi.

# Mlinzi Siha adaiwa kumuua mwananchi, polisi yamshikilia

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MLINZI wa watawa wa Shirika la Kazi ya Roho Mtakatifu anadaiwa kumpiga risasi na kumuua mkazi wa Kijiji cha Mlangoni, Kata ya Gararagua Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Nicholas Nzota.

Taarifa za awali zinaeleza kuwa Nzota, ambaye ni Mkazi wa Kitongoji cha Kilari, alikwenda karibu na shamba la watawa hao (Holly Spirit Sisters) linalomilikiwa na Kanisa Katoliki, Jimbo la Moshi.

Alipokuwa katika eneo hilo alisikia sauti za wanawake wakipiga yowe kuashiria kuomba msaada, ndipo alipokwenda hadi kwa walinzi hao na kuhoji sababu za kuwashikilia watu hao

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Dk. Christopher Timbuka, alisema tukio hilo la mauaji limetokea Oktoba Mosi mwaka huu, majira ya saa 1:00 usiku karibu na Hospitali ya Charlotte.

Kwa mujibu wa Dk. Timbuka, walinzi wa shirika hilo la watawa, walikuwa wamewashikilia mateka wanawake wawili waliowakuta eneo la mpakani mwa hospitali hiyo, jambo ambalo lilileta vurugu baina ya wananchi na walinzi hao.

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, Kaimu Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Yahaya Bwanamdogo, alisema tayari wanamshikilia mlinzi huyo kwa ajili ya mahojiano zaidi.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mlangoni, Ezekiel Mloli, alisema ni kweli alipokea taarifa kwamba kuna mtu amepigwa risasi mpakani mwa shamba la watawa hao na shamba linalomilikiwa na chama cha msingi, na alipofika eneo la tukio aliukuta mwili wa Nzota ukiwa chini.

"Baada ya kuuona, nilitoa taarifa Kituo Kikuu cha Polisi Sanya Juu, walikuja na kuuchukua mwili wa marehemu kuupekeka Hospitali Maalum ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibongoto kwa ajili ya kuhifadhi.

"Unajua marehemu (Nzota), alifika katika eneo hilo baada ya kusikia sauti za kinamama wakiomba msaada.

...Mtu huyo huyo, hii ni mara ya pili kupiga watu risasi. Miezi minne iliyopita alimpiga kijana mwingine risasi ya mguu na kuuvunja. Ameona haitoshi amerudia tena na kuua mwananchi mwingine kwa risasi. tunaomba sheria ichukue mkondo wake maana tumechoka."

Mei mwaka huu, katika eneo hilo hilo, karibu na shamba la watawa wa Shirika la Kazi ya Roho Makatibu, wananchi wanadai mlinzi huyo huyo, alimpiga risasi ya mguuni mkazi wa Magadini, Boke Mollel, akimtuhumu kutaka kumnyang'anya silaha, wakati wa ukamataji wa mifugo yake ikiwamo ng'ombe alioelezwa waliingia ndani ya shamba hilo. Kutokana na matumizi hayo ya nguvu, hasa matumizi ya bunduki, wakazi wa Kitongoji cha Kilari, akiwamo Beatrice Shoo, wameiomba serikali na vyombo kuingilia kati sakata hilo, kwa kuwa hata silaha iliyotumika Mei kujeruhi hawajui imerejeaje mikononi mwa mlinzi huyo.

Katika mkutano wa dharura ulioitishwa leo (jana) kijijini humo, Mbunge wa Siha na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, amewasihi wananchi wa Kijiji cha Mlangoni na hasa Kitongoji cha Kilari, kuwa watulivu, wakati jambo hilo linashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Dk.Mollel alisema: "Nawaombeni utulivu na uvumilivu mliouonyesha toka jana, lililotokea tatizo hili muendelee kuhudumisha najua ni vigumu.

...Lakini hakuna kitu kizuri kama kuwa na uvumivu kwa jambo kubwa kama hili. Mwananchi mwenzetu amepoteza maisha na kuacha familia, ila tupo pamoja kuhakikisha haki inapatikana."



Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo (kushoto), akiwa na wataalamu kutoka Halmashauri ya Jiji la Arusha pamoja na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakikagua daraja la Engosengiu Kata ya Sinoni jijini humo jana, ambalo ujenzi wake umekamilika. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Gambo: Hamnikwamishi mimi bali mnaikwamisha CCM

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MBUNGE wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, amesema watu wanaokwamisha maendeleo katika jimbo hilo watambue kuwa siyo yeye wanamkwamisha, bali wanakikwamisha Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambacho kimemwamini na kumpa dhamana ya kugombea kuwakilisha wananchi.

Lema aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Sinoni, kueleza kuwa wapo baadhi ya watu wanaokwamisha maendeleo lakini amejitoa kuwakilisha wananchi kama ambavyo walimuamini na kumpa kura.

"Wakati tukipambana ili mpate maendeleo wapo wanaopambana kukwamisha, ila watambue tu kuwa hawamkwamishi mbunge, diwani wala wenyeviti bali wanakikwamisha Chama Cha mapinduzi ambacho kimenipa dhamana ya kugombea" alisema Gambo.

Baadhi ya wananchi wa kata hiyo walieleza matatizo yanayowakabili katika Kata hiyo ikiwemo kero ya maji ambapo wamedai kubambikiziwa bili kubwa pamoja na maji kuwa machafu yanayotoka katika AUWSA. Lembrisi Lekashu ni mkazi wa Engosengiu kutoka kata hiyo alisema upatikanaji wa maji yamekuwa kero ambapo wananchi wamekuwa wakibambikiziwa bili kubwa ili hali maji hayatoki mara kwa mara.

Naye Diwani wa kata hiyo, Michael kivuyo aliwataka wananchi kutoa ushirikiano na endapo kama watasikia eneo linalouzwa kuanzia ekari mbili watoe taarifa ili halmashauri iweze kununua kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya pamoja na shule.

Katika ziara hiyo, Gambo alikagua kivuko cha watembea kwa miguu cha Engosengiu, barabara inayotarajiwa kuwekwa lami yenye urefu wa kilomita nne na nusu ya Engosheratoni, 000000000

## Vijana watengewa bil.5/- kuwezeshwa kiuchumi

Na Jaliwason Jasson, BABATI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Ajira, Kazi, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, amesema kwa mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetoa Sh. bilioni tano, kati ya Sh. bilioni tisa zilizotengwa kwa ajili ya kuwawezesha vijana kujiinua kiuchumi.

Aliyasema hayo jana, katika Mji wa Babati mkoani Manyara, baada ya kukagua uwanja mpya utakaotumika kuhitimisha mbio za Mwenge wa Uhuru, Oktoba 14 mwaka huu.

Alisema serikali imeishawawezesha Sh. bilioni moja kutokana na marejesho Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo imeishatoa Sh. bilioni 2.8 kwa vijana.

Aidha, alisema serikali inatakiwa kutoa Sh.bilioni tisa ili kuwajengea ujuzi vijana ambapo inaangalia sekta za utalii, mapishi na ujasiriamali.

Vilevile, alisema katika mwaka wa fedha 2023/24 watawaingiza vijana 1,500 ambapo bajeti ya mwaka huu ni Sh. bilioni tisa ila wameshapewa Sh. bilioni tano.

Awali, Katibu Mku, Ofisi ya Waziri Mkuu, Cyprian Luhemeje, aliwaomba vijana wote kufika Manyara ili kwenye wiki ya vijana wajadiliane namna ya kupata ajira ndani na nje ya nchi.

Luhemeja alisema wakifika wataweza kupunguza kulalamika maana watazioná fursa za ajira.



# CCM: Uchaguzi Serikali za Mitaa mwakani ni 'mfupa mgumu'

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, kimekili kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika 2024 utakuwa ni mgumu.

Kimesema ugumu huo unatokana na vyama vya siasa kupewa uhuru wa kufanya mikutano ya siasa.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Mabala Mlolwa, alipofanya ziara katika kata za mkoani hapa, akiongea na viongozi wa serikali za mitaa na wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM ngazi ya kata kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi huo.

**Sitarajii kuona CCM inapoteza hata kijiji kimoja wala kitongoji katika uchaguzi huo utakaofanyika mwakani.**

Mlolwa alisema Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024 siyo wa kufanyia mzaha, bali wanatakiwa kujipanga ili kuhakikisha wanatetea viti vyao visienda kwa wapinzani.

"Rais Samia Suluhu Hassan amefungua demokrasia hapa nchini, hivyo katika uchaguzi huu tunapaswa kujipanga kwa kuanza maandalizi mapema ili tupate ushindi wa kishindo na ushindi huo ndiyo utatufanya tushinde tena Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025," alisema Mlolwa.

Alisema wanachopaswa kufanya viongozi wa serikali za mitaa ni kuendelea kufanya mikutano ya hadhara ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi ili waendelee kuaminika kwa wananchi.

Aidha, aliwataka pia wajumbe wa CCM ngazi ya kata, wanapokuwa wakipitisha wagombea kwenye kura za maoni ambao watapeperusha bendera ya chama hicho katika uchaguzi huo, wachague wagombe wenye sifa wanaokubalika na wananchi.

Alisema hatarajii kuona CCM inapoteza hata kijiji kimoja wala kitongoji katika uchaguzi huo utakaofanyika mwakani.

Naye Mbunge wa Solwa, Ahmed Salum, alisema kero za wananchi ambazo zilikuwa zikimsumbua tangu achaguliwe mwaka 2005 ikiwamo shida ya maji, umeme, huduma za afya, miundombinu ya barabara na madaraja amezitatua.

Alisema hadi kufikia mwaka 2030 vijiji vyote 126 Solwa hakutakuwa na shida hizo tena, bali litabakia tu suala la kuongeza vyumba vya madarasa kwa sababu ni hitaji la kila mwaka.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa (kulia), akionyesha kwa waandishi wa habari, mkoani humo jana, baadhi ya vifaa vya uvuvi vinavyodaiwa kuwa ni vya wizi zikiwamo nyavu za uvuvi haramu aina ya kokolo vilivyokamatwa katika msako wa wiki moja uliofanywa na jeshi hilo. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Jeshi la Polisi lakamata shehena ya vifaa vinavyotumika kwa uvuvi haramu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limekamata shehena ya vifaa vya uvuvi vinavyosadikiwa kuwa vya wizi pamoja na vingine vinavyotumika katika uvuvi kinyume cha sheria.

Vitu vilivyokamatwa ni pamoja na mashine za boti 12, mitumbwi 18 iliyokutwa na nyavu 1,202, mitumbwi minne isiyokuwa na namba za usajili kinyume cha sheria ambayo pia ilikutwa na nyavu haramu 10.

Akitoa taarifa hiyo juzi kwa waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa, alisema miongoni mwa nyavu 1,202 zilizokamatwa na jeshi hilo 387 zimetambuliwa na watu walioibiwa.

Vilevile alisema kuwa katika mikutano ya hadhara waliyoifanya katika maeneo mbalimbali mkoani Mwanza walibaini uwepo wa kero ya vitendo vya wavuvi kuvamiwa nyakati za usiku na kunyang'anywa mali zao.

"Katika msako huo kupitia polisi wetu pamoja na idara ya uvuvi mkoani hapa tumefanikiwa kuwakamata watu watano wanaotuhumiwa kuhusika na uvamizi huo katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Ziwa Victoria," alisema SACP Mutafungwa.

Kadhalika, alisema baadhi ya wavuvi waliokuwa wakitumia nyavu zilizokamatwa walizikimbia hali inayoashiria kuwa walikuwa wakizitumia kinyume na sheria.

Alisema operesheni hiyo endelevu ilianza Septemba 26 ikifanyika katika maeneo ya visiwa vya Bezi, Ikulu, Ito, Ntama na kwenye mialo mingine sita iliyopo katika Halmashauri ya Ilemela pamoja na Nyamagana.

Naye Ofisa Mfawidhi wa Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvivi Kanda ya Ziwa Victoria, Farah Bulongo, aliwataka wavuvi wote kufanya uvuvi wenye tija ili kuhakikisha sekta ya uvuvi inakuwa endelevu na kuacha matumizi ya zana haramu.

## H'shauri yapewa gari kusimamia utekelezaji miradi

**Na Timothy Itembe,** MARA

HALMASHAURI ya Tarime Vijijini imekabidhiwa gari la Sh. milioni 160 kutoka kampuni ya uchimbaji wa dhahabu Barrick Nyamongo kwa kushirikiana na Kampuni ya Twiga.

Lengo la kupewa gari hilo ni kusimamia kukamilisha miradi ya kurudisha kwa jamii (CSR) inayodaiwa kusuasua.

Inaelezwa kuwa miradi mingi ya CSR katika halmashauri hiyo imekuwa ikikwama kutokana na kutokukaguliwa kwa wakati na kusimamiwa ipasavyo na halmashauri kutokana na kukosa usafiri wa kuifikia miradi hiyo.

Akikabidhi gari hilo aina ya Toyota Land Cruiser, Rais wa Kampuni ya Barrick, Mark Brisiton, aliitaka halmashauri hiyo kutumia gari hilo kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuhakikisha kila kinachopelekwa kwa jamii kinawafikia walengwa.

Naye Meneja wa Mgodi wa Barrick Nyamongo, Apolnary Lyambiko, alisema limenunuliwa kutokana na fedha za mapato ya ndani ya mgodi huo na Kampuni ya Twiga.

## Kampuni ya tumbaku yalipa wakulima Bil.152/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Alliance One Tobacco Tanzania imelipa Sh. bilioni 152.4 kwa wakulima wa tumbaku kutoka katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Mwanza na Kigoma katika msimu wa mavuno wa mwaka 2022/2023.

Akizungumza na wawakilishi wa wakulima 13,000 walioiuzia tumbaku kampuni hiyo, Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Tumbaku, David Mayunga, alisema kwa sasa jopo la viongozi wa kampuni hiyo wameweka mikakati ya kuwatumia maofisa ugani wa kampuni hiyo kutoa elimu zaidi kwa wakulima walioingia nao mikataba wa uzalishaji tumbaku.

Alisema hali hiyo inatokana na kuwapo kwa madai kwa baadhi ya wakulima kuweka takataka katika tumbaku kama njia ya kuongeza kilo wakati wa uuzaji.

Alisema vitendo hivyo vya kuweka uchafu kwa lengo la kuongeza kilo linaathiri na kuongeza gharama za kuchambua tumbaku inapofika kiwandani kwa ajili ya kuchakatwa.

Mayunga alisema tabia ya baadhi ya wakulima kuchanganya madaraja ya tumbaku, kuweka mawe, kandambili, magodoro, vitambaa, manyoya ya ndege ili kuongeza kilo wakati wa kuuza sio tabia nzuri bali inapelekea kampuni kupata hasara na kushusha thamani ya zao hilo sokoni.

Alisema katika msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023 kampuni imewalipa wakulima Dola za Marekani milioni 60 (Sh.bilioni 152.4) ndani ya siku nne tangu iliponunuliwa tumbaku kutoka kwa wakulima.

Mayunga alisema kampuni hiyo imelipa ushuru wa halmashauri za wilaya Sh. bilioni 4.6, ushuru wa vyama vya msingi Sh. bilioni 4.7, ushuru wa vyama vikuu Sh. bilioni mbili.



Ukurasa 12

**Mbarali wanapohitimisha mchakato kidemokrasia**



Ukurasa 13

Ndivyo ubadhirifu fedha umma ulivyo ukatili kwa Watanzania


# siasa

JUMATANO OKTOBA 4, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**MARTIN FAYULU**

**Mpinzani atakayemkaba Rais Tshisekedi Desemba**

# 'Hazina ya taifa' inautaka uwakilishi bungeni, barazani

• Hawa ni wazee wanaoomba kuthaminiwa, huduma bora



Baadhi ya wazee wakifuatilia maadhimisho ya siku yao mjini Zanzibar. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika, ZANZIBAR**

OKTOBA mosi kila mwaka, ni kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani ambayo safari hii wazee wa Zanzibar kwa niaba ya wenzao wa taifa hili, wanaomba kupewa nafasi za kuwa na wawakilishi katika vyombo vya kutunga sheria, bungeni na Baraza la Wawakilishi.

Mzee Issa Kidali, aliyesoma risala kwa niaba ya wazee wenzake mbele ya mgeni rasmi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Othman Masoud Othman, akiwasilisha mbele yake ombi hilo.

Aidha, wanaikumbusha serikali, wenye vyombo vya usafiri na taasisi zinazosimamia usafirisha kuhusu maelekezo ya kulipa nusu ya nauli kwa wazee, watu wenye ulemavu na wanafunzi.

Ni katika ukumbi wa mikutano wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), kilichopo Tunguu, mkoa wa Kusini Unguja, akisema wakiwa na uwakilishi katika vyombo hivyo, utafanikisha kupunguzia kero, akiongeza kuwa wanaomba kupatiwa nafasi maalumu za uwakilishi bungeni na barazani.

"Kwa mara nyingine tunakumbusha Sheria ya Usafiri Barabarani Namba 7 ya mwaka 2003 ambayo imekubali wazee, wanafunzi na watu wenye ulemavu kulipa nusu gharama katika vyombo vya usafiri kama daladala, lakini hili suala halizingatiwi, hasa wazee kulipa nauli kamili," anakumbusha.

Mbali na hilo anapaaza sauti ya wazee kuomba lianzishwe dirisha maalum la kusaidia wazee sehemu za huduma kama hospitalini, benki, vyombo vya usafiri na popote zinapotolewa huduma za kijamii.

Mwakilishi huyo wa wazee anasema, wakiwa na uwakilishi kwenye vyombo vya kutunga sheria, itakuwa ni rahisi kufikisha kero zao moja kwa moja sehemu hizo badala ya kuzisemea nje kama ilivyo sasa.

Mzee Kidali, anaainisha msururu wa kero zao kuwa ni pamoja na mipango ya sekta kutozingatia kikamilifu hali na maslahi yao, ikiwamo bima ya afya kwa wazee, huku akitaja nyingine kuwa ni mafao yanayotolewa kwao kupitia pensheni jamii kutokuwa sawa.

Anafafanua kuwa haijawa sawa kwenye malipo, kwa kuwa walipaji wanapofika vituoni wana haraka ya kuondoka, na kwamba kitendo hicho kimesababisha ugumu kwa wazee kupata fedha za mwezi uliopita.

"Lakini pia katika kitengo cha pensheni jamii hakuna dawati maalum la malalamiko katika Wizara ya Fedha. Aidha, huduma za afya kwa wazee hazijazingatia vya kutosha hali na magonjwa ya wazee, pia dawa zinapatikana, lakini madaktari na wahudumu wa wazee hawapo.

Kidali anaainisha kero nyingine kuwa ni lishe duni ya wazee, hasa wanaoishi vijijini, hawaangaliwi vizuri na pia wanadhalilishwa kwa tuhuma za uchawi.

"Wazee wanakosa misaada stahiki katika maeneo mbalimbali kama benki, na baadhi ya maeneo ya kutolea huduma nyingine, tunahitaji vitambulisho maalum vitolewe haraka ili wapate huduma za kijamii, kuanzia usafiri, afya na fedha bila usumbufu," anasema.

**WAZEE WATAMBULIWA**

Akizungumza kwa niaba ya Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Othman Masoud Othman, anasema hadi kufikia Septemba mwaka huu, serikali imetoa vitambulisho 28, 668 kwa wazee wote wa umri wa zaidi ya miaka 70.

Anawaambia wazee na wadau wanaoshiriki maadhimisho hayo kuwa , lengo la kufanya hivyo, ni kutaka viwasaidie kupata kirahisi huduma muhimu za kijamii ikiwamo usafiri wa umma, afya, kuingia kwenye viwanja vya michezo vya serikali na pensheni ya jamii.

Makamu wa Rais anasema mbali na hilo, kwa kutambua na kuthamini mchango wa wazee wa kuleta maendeleo ya nchi, serikali imeongeza kiwango cha pensheni ya jamii kutoka sh. 20,000 hadi 50,000.

Anaeleza kuwa hadi kufikia mwezi uliopita jumla ya wazee 29, 307 wamesajiliwa kwa ajili kupata pensheni ya jamii, Unguja wakiwa 17,482 na Pemba 11, 825 na kwamba kwa kiasi kikubwa, pensheni imesaidia wazee kuimarisha maisha yao na familia zao ikiwamo kuanzisha shughuli mbalimbali za kujipatia kipato.

Makamu wa Rais Dk. Othman, anawaagiza watendaji wanaoshughulikia pensheni ya jamii kushirikiana kwa karibu ili kusaidia kufanikisha lengo la serikali la kuondoa changamoto zinazojitokeza wakati wa usajili hadi kupokea pensheni.

**INAENDELEA UK. 14**

# Mbarali wanapohitimisha mchakato wa kidemokrasia

Na Mroki Mroki

UCHAGUZI ni mchakato rasmi wa kufanya maamuzi ambapo raia wanamchagua mtu au watu wa kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi kwenye ofisi ya umma lakini katika taasisi nyingine zikiwamo za binafsi, asasi za kiraia na za kidini.

Umekuwa mfumo wa kawaida ambao unatumika katika zama hizi za demokrasia ya uwakilishi katika nchi mbalimbali duniani na mfumo huu kwa baadhi ya mataifa umekua ukifuatwa tangu karne ya 17. Tanzania ni moja ya nchi za kidemokrasia inayofuata mfumo wa siasa ya vyama vingi.

Itakumbukwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, ulirejeshwa mwaka 1992 baada ya kufutwa mwaka 1964 kwa upande wa Zanzibar na mwaka 1965 kwa Bara. Tangu kurejeshwa kwa mfumo huo, jumla ya chaguzi sita zimefanyika kila baada ya miaka mitano kuanzia 1995 hadi 2020.

Mbali na chaguzi sita zilizowahi kufanyika kila baada ya miaka mitano kuanzia 1995 hadi 2020 pia kumekua na chaguzi ndogo za ubunge na udiwani ambazo zimekuwa zikifanyika mara kwa mara panapotokea aidha kifo cha mbunge jimboni au diwani kwenye kata.

Jimbo la Mbarali lililopo mkoani Mbeya ni miongoni mwa majimbo yaliyofanya uchaguzi mdogo kufuatia kifo cha mbunge wake Francis Mtega.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa mujibu wa katiba na sheria za uchaguzi imepewa jukumu la kusimamia, kuratibu na kuendesha mchakato mzima wa uchaguzi nchini. Ilitimiza kikamilifu jukumu lake katika kuandaa mchakato mzima wa uchaguzi mdogo jimboni humo na katika kata sita.

Tume ilitangaza ratiba nzima ya uchaguzi mdogo ambapo wagombea walitakiwa kuchukua fomu kuanzia Agosti 13 hadi 19, 2023, siku ya uteuzi ilikuwa Agosti 19, 2023 na kampeni za uchaguzi zilifanyika kuanzia Agosti 20 hadi 18 Septemba 18.

Wagombea waliopendekezwa na vyama vyao vya siasa kugombea kiti cha ubunge walitakiwa kujaza na kuwasilisha fomu za uteuzi katika ofisi za uchguzi katika jimbo na kata husika.

Aidha, wagombea ubunge waliwasilisha fomu za uteuzi katika ofisi za wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo na wagombea udiwani kwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata. Fomu za uteuzi za wagombea wote ziliwasilishwa siku ya uteuzi kabla ya saa



Mbunge mteule wa Mbarali Bahati Ndingo , baada ya kutangazwa mshindi. PICHA: MROKI MROKI

10:00 jioni kwa mujibu wa sheria. Wakati wote wa kampeni wagombea walitakiwa kuzingatia sheria, kanuni za uchaguzi, maadili ya uchaguzi na ratiba za kampeni.

Jambo hili la uzingatiaji wa sheria, kanuni za uchaguzi, maadili ya uchaguzi na ratiba za kampeni lilizingatiwa kikamilifu na vyama vyote vilivyoshiriki uchaguzi mdogo Mbarali na kata sita na hapakua na malalamiko yoyote yaliyowasilishwa katika kamati za maadili ngazi ya kata, jimbo wala taifa.

Katika uchaguzi huu mdogo wagombea 13 kutoka vyama vya siasa 14 vyenye usajili waliteuliwa kuwania kiti cha ubunge Mbarali na vyama vyao kwenye mabano ni Halima Magambo (AAFP), Oswad Mndeva (DP), Zavely Seleka (UDP), Exavery Mwataga (CCK), Mary Daudi (UPDP), Modestus Kilufi (ACT-WAZALENDO), Morris Nkongolo (TLP), Hashim Mdemu (ADC), Fatuma Ligania (NLD), Mwajuma Milambo (UMD), Bahati Ndingo (CCM), Hussen Lusewa (ADA-TADEA) na Bariki Mwanyalu (DEMOKRASIA MAKINI.

Aidha, vyama vya siasa 17 vilijitokeza kuchukua fomu kwaajili ya kuwania nafasi za udiwani katika kata sita za Tanzania Bara na wagombea 45 waliteuliwa kuwania nafasi hizo.

Kata zilizofanya uchaguzi mdogo ni Nala (Dodoma), Mfaranyaki (Manispaa ya Songea), Mwaniko (wilayani Misungwi), Old Moshi Magharibi (Wilaya ya Moshi), Marangu Kitowo ( Rombo) na Mtyangimbole (Wilaya ya Madaba).

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, imepewa jukumu la kutoa elimu ya mpigakura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi au asasi zinazotoa elimu hiyo.

Elimu ya mpiga kura katika jimbo la Mbarali na kata sita ilitolewa kwa wananchi kwa lengo la kuwawezesha kuielewa sheria, kanuni na taratibu za mchakato wa uchaguzi.

Elimu hiyo iliyolenga kuwahamasisha wananchi kutumia haki yao ya kikatiba katika kujitokeza kupiga kura na kuchagua viongozi wanaowataka, ilitolewa kwa kutumia vipindi vya redio, makala magazetini na na matangazo mbalimbali.

Wananchi walijitokeza katika mikutano ya kampeni za vyama vya siasa ambavyo vilikua vikinadi wagombea na sera zao, hatimaye baada ya kusikia sera, kuzichambua na kuzitafakari waliamua kutumia haki yao ya kidemokrasia na kuchagua viongozi wanaowataka.

Jimbo la Mbarali lilikua na wapiga Kura walioandikishwa katika Daftari la kudumu la

> Wagombea waliopendekezwa na vyama vyao vya siasa kugombea kiti cha ubunge walitakiwa kujaza na kuwasilisha fomu za uteuzi katika ofisi za uchguzi katika jimbo na kata husika.

Wapiga Kura wapatao 185,836 na vituo 490 vya kupiga Kura.

Kati ya wapigakura 185, 836 , waliojitokeza ni 56,662 na kupiga kura katika uchaguzi huo wa ubunge kura halali zilikuwa 56,095 na kura zilizoharibika zilikuwa 567.

Baada ya zoezi la kupiga kura na kuhesabu kura kukamilika , Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Mbarali, Missana Kwangura anatangaza matokeo Septemba 20, 2023 akimtangaza, Bahati Ndingo wa CCM kuwa mshindi baada ya kupata kura 44,334 akifuatiwa na Modestus Kilufi wa ACT-WAZALENDO aliyepata kura 10,014.

Wagombea wengine ni, Halima Magambo wa AAFP aliyepata kura 336, Bariki Mwanyalu wa Demokrasia Makini aliyepata kura 207, Hashim Mdemu wa ADC kura 173, Zavely Seleka wa UDP 158, Husseni Lusewa wa ADA-Tadea kura 155, Morris Nkongolo wa TLP kura 139 na Oswald Mndeva wa DP kura 130.

Wagombea wengine ni Exavery Mwataga wa CCK kura 118, Mwajuma Milambo wa UMD na Mary Daudi wa UPDP walipata kura 113 kila mmoja na Fatuma Ligania wa NLD alipata kura 105.

Baada ya kutangazwa matokeo hayo, baadhi ya wagombea wanazungumza na kutoa pongezi kwa mwenzao aliyeshinda na kumuahidi ushirikiano katika kuwatumikia wana Mbarali.

Aliyekuwa mgombea wa AAFP, Halima na wa CCK Mwataga kwa pamoja wanampongeza mshindi na NEC kwa usimamizi na kuongeza kuwa uchaguzi ulikuwa huru na haki na umemalizika kwa amani.

"Tunamshurukuru msimamizi wa uchaguzi , Missana Kwangura amesimamia vyema uchaguzi huu tangu tunachukua fomu mpaka hapa tulipofika kwani uchaguzi umekuwa huru na wenye amani na ulikuwa wa haki, ...Leo nimeshika nafasi ya tatu lakini naamini ipo siku nitakuwa mshindi,"anasema Halima.

"Siasa sio vita, ni mchakato tu baada ya mambo haya yote tulishasema tutakumbatiana maana kasungura kalikua kadogo mwenzetu kamega kubwa, hivyo tunampongeza maana sote tulikuwa na nia ya dhati ya kwenda mjengoni bungeni hivyo ukifika walau tualike nasi tufike, " anasema Mwataga.

Mshindi wa kiti cha ubunge Mbarali Bahati anapata fursa ya kuzungumza na kuipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa uratibu na usimamizi wa uchaguzi huo lakini pia akiwashukuru wananchi kwa kumchagua.

"Ninawashukuru tume kwa uratibu na usimamizi wao , shukrani zangu kwa wana Mbarali kwa kuniamini na kunichagua. Kwa kushirikiana na viongozi wenzangu naamini tutakwenda kufanya kazi iliyotukuka kwa ajili ya wapigakura wetu. Kwa wagombea wenzangu na ninawaahidi tutaendelea kushirikiana kwa maslahi ya watu wa Mbarali,"anasema Bahati.

**Mwandishi ni Ofisa Habari Msaidizi Mwandamizi NEC.**



Vyoo vibovu katika shule za msingi na sekondari vinavyosababisha wanafunzi na walimu kujisaidia vichakani, ni matokeo ya kufuja fedha za umma kwenye elimu. PICHA: IPP MEDIA.

# Ndivyo ubadhirifu fedha umma ulivyo ukatili kwa Watanzania

**Na Reubeni Lumbagala,**
DODOMA.

ZIARA ya Rais Samia Suluhu Hassan, mkoani Mtwara, imekutana na ubadhirifu wa fedha za miradi ambao unaweza kuitwa ukatili kwa watanzania wengi maskini.

Ajenda ya wananchi ni maendeleo, watanzania hawataki blahblah kutoka kwa viongozi, wanachohitaji ni maisha bora ambayo ni maendeleo yanayogusa ustawi wao.

Viongozi wanaochaguliwa na kuteuliwa, wajibu wao namba moja ni kuwatumikia wananchi kwa kuhakikisha wanatimiza wajibu na majukumu yao kikamilifu ili azma ya serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo iweze kutimia.

Pamoja na umuhimu wa upatikanaji wa rasilimalifedha kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo, usimamizi na uratibu mzuri wa matumizi ya fedha hizo ni jambo la msingi na muhimu mno.

Usimamizi mbovu, matumizi mabaya na ufujaji wa fedha za miradi ya maendeleo ni adui wa kufikia azma ya serikali ya kufikisha maendeleo kwa wananchi wake.

Kwahiyo, kama serikali itatimiza wajibu wake wa kutafuta fedha za miradi lakini kukawa na matumizi mabaya na utafunaji wa fedha hizo, maendeleo ya wananchi hayawezi kufikiwa kama ilivyokusudiwa na umaskini unazidi kuongezeka.

> “Usimamizi mbovu, matumizi mabaya na ufujaji wa fedha za miradi ya maendeleo ni adui wa kufikia azma ya serikali ya kufikisha maendeleo kwa wananchi wake.

Kwa ujumla ubadhirifu na ufujaji wa fedha za miradi ni ukatili kwa wananchi kwani unasababisha kucheleweshewa maendeleo na pia miradi hiyo kutekelezwa chini ya viwango kutokana na kukosekana kwa thamani halisi ya pesa (value for money) inayotakiwa.

Jambo muhimu ambalo viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia matumizi ya fedha za umma kufanikisha miradi ya maendeleo wanapaswa kufahamu ni kuwa pesa za Watanzania si mali yao, ni za wavuja jasho, maskini ambazo zinapaswa kutumika kikamilifu kutekeleza mradi na mipango iradi iliyokusudiwa kwa manufaa ya Watanzania wote leo na vizazi vijavyo.

Rais Samia akiwa wilayani Tandahimba mkoani Mtwara anakemea matumizi mabaya ya fedha za miradi ya maendeleo, akisema viongozi na vyombo vingine havifanyi kazi ipasavyo, jambo linalosababisha ubadhirifu wa pesa ambazo zinalenga kuleta maendeleo.

“Inakuwaje fedha za miradi zinatumika vibaya inaonyesha viongozi wa eneo hilo wameshindwa kusimamia udhibiti wa matumizi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

“Nasubiri taarifa ya TAKUKURU niweze kuchukua hatua zaidi za juu, lakini najiuliza uwepo wa madiwani, wakuu wa wilaya, kamati za siasa CCM inakuwaje fedha zije zitumike vibaya?” anahoji Rais Samia.

Wito wa Rais Samia ni viongozi wa ngazi zote kuanzia mkoa, wilaya, tarafa, kata, vijiji, vitongoji, mitaa na wananchi wote kushirikiana kufanikisha matumizi mazuri ya fedha za miradi ili wananchi waweze kunufaika na miradi hiyo, hatimaye maendeleo yaweze kufikiwa.

Wananchi wanataka kuona ahadi zilizoahidiwa na viongozi wakati wa uchaguzi zinatekelezwa ipasavyo , tena si vyema wenye dhamana kujisahaulisha au kuwa wabadhirifu wa fedha hizo, kwani wanakwamisha moja kwa moja miradi hiyo na hivyo kusababisha wananchi kuendelea kupata shida kutokana na kushindwa kutatuliwa kero zinazogusa maisha yao.

Matumizi mabaya ya fedha za umma ni ukatili kwa watanzania, kwani unaathiri moja kwa moja maisha yao, mathalani, wanakosa vituo vya afya, madaraja wanatembelea barabara za vumbi zisizokwanguliwa wala kusindiliwa.

Wanafunzi hawana vyoo, wanajisaidia vichakani, porini ,wanasongamana darasani, hawana vitabu wala walimu kwa vile fedha zinaishia mikononi mwa wachache.

Kinamama na watoto wanasababishiwa vifo visivyo vya lazima licha ya kwamba maisha yao yangeweza kuokolewa kama wangepata huduma bora za afya hospitalini.

Viongozi walafi kumbukeni ukosefu wa huduma za maji unaweka rehani maisha na ndoa za wananchi kwani wanawake wanatumia muda mwingi kutafuta maji na hivyo kusababisha hata kuuliwa na wanyama wakali mfano fisi lakini migogoro na waume zao ikiongezeka.

**TAMBO, DHARAU**

Wakati hayo yanatokea viongozi na wasimamizi wa miradi ya umma wanajenga majumba makubwa au msururu wa mijengo wakiita ‘apatments’ kila mkoa ili kupangisha na kujitajirisha.

Tena wanatamba kuwa mtumishi wa serikali akijenga hasimami wala hapoi. Nyumba ni mwanzo mwisho kwa muda mfupi wakizungushia huwa mkubwa, kuweka mapambo na nakshi za kila namna. Ni tambo na majigambo yao mitaani.

Wapo wanaojenga vituo vya mafuta, kununua magari ya kila na kuyaegesha uwani tena wakiishi maisha ya kifahari kwa wizi wa fedha umma unaowanyong’onyeza wengine wanaosota na kuendelea kubaki fukara.

Kutokana na kiu kubwa ya Rais Samia ya kuwatumikia wananchi kwa kuhakikisha wanapata huduma bora, aliwaonya viongozi kuwa tamaa za mali hazisaidii maana watakufa na kuziacha na kusisitiza kuwepo na hofu ya Mungu.

Anawakumbusha kuwa waliopewa dhamana ya kusimamia mipango na miradi ya wananchi hawapaswi kuwa kikwazo cha kutimiza kiu hii ya kufikia maendeleo endelevu.

Ni vyema kila kiongozi atamani kuacha alama inayoishi kwa wananchi katika eneo lake la utawala kwa kuhakikisha anashiriki kikamilifu katika usimamizi mzuri wa fedha za miradi ya maendeleo ili wananchi wafurahie maendeleo.

Wakumbuke kuwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni neema kwa kizazi cha sasa na kijacho; hivyo basi, wakati viongozi wakiwajibika kusimamia vyema fedha za miradi ya maendeleo, wananchi kwa upande wao wanawajibika kuitunza miradi hiyo kwa maslahi mapana ya taifa.

Viongozi msisahau kuwa kutokana na ajenda ya wananchi kuwa maendeleo, ndiyo maana serikali kwa kushirikiana na wadau wa hufanikisha upatikanaji wa fedha ambazo ni nyenzo muhimu ya kufikia maendeleo hayo kupitia utekelezaji wa miradi na shughuli za uwekezaji kimikakati kuanzia kilimo, uvuvi, ufugaji na huuma za kijamii.

Mapato na fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo zinapatikana kupitia kodi zinazolipwa na wananchi, mikopo na misaada ya wahisani. Upatikanaji wa raslimalifedha unachagiza utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo kama vile ujenzi wa shule, hospitali, nyumba na ofisi za serikali, miradi ya maji, umeme, miundombinu, ununuzi wa pembejeo za kilimo, ufugaji na uvuvi na viwanja vya michezo. Miradi hii ya maendeleo haiwezi kufanikiwa bila uwepo wa raslimalifedha.

Viongozi hao wajiulize itamfaa nini mwenye dhamana kuiba, kujikusanyia mali na utajiri mwingi na kusababisha mamilioni ya wananchi kuishi kinyonge na kuteseka? Wakumbuke haki ya wenye haki haipotei na ipo siku watalipa wizi na ubadhirifu huo pengine mara 100.

**Mwandishi ni mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Dodoma. Maoni: 0620 800 462.**

JUKWAA LA VIONGOZI

MARTIN FAYULU

# Mpinzani atakayemkaba Rais Tshisekedi uchaguzi Desemba

**Na Christina Mwakangale**

KIONGOZI wa upinzani nchini DRC, Martin Fayulu amethibitisha kugombea urais kwenye uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Desemba 20, mwaka huu.

Atashindana na Rais Felix Tshisekedi, aliye madarakani tangu mwaka wa 2019, ambaye pia anawania muhula wake wa pili.

"Muungano wa LAMUKA umeamua kuwasilisha ugombea wangu kwenye uchaguzi wa rais," Martin Fayulu anawaambia waandishi wa habari mjini Kinshasa.

Tangu Julai, mwaka jana, chama chake cha ECIDE ambacho kinashiriki kwenye muungano wa LAMUKA, kilikuwa kimemteua Martin Fayulu kuwa mgombea wake rasmi kwenye uchaguzi ujao wa rais.

Baada ya Tume Huru ya Uchaguzi (CENI) kutupilia mbali madai ya viongozi wa upinzani kuhusu mchakato wa uchaguzi, Fayulu, mmoja wa viongozi hao tayari amethibitisha kushiriki kinyang'anyiro hicho.

Miongoni mwa madai waliyoyatoa walipokutana na mkuu wa CENI, Denis Kadima, siku chache zilizopita, upinzani ulisisitiza kuwa daftari la uchaguzi likaguliwe na kampuni huru yenye umaarufu na ujuzi wa kimataifa, lakini CENI iliyatupilia mbali masharti hayo.

Julai, mwaka huu, akizungumza na waandishi wa habari mjini Kinshasa, Fayulu, alikataa kabisa kushiriki katika kile alichokielezea kuwa ni maandalizi ya udanganyifu ya uchaguzi na akatishia hata kuwahamasisha wakongo kudai mamlaka yao kupitia maandamano.

"Hatutawasilisha maombi yetu ya ugombeaji kwani tunakataa kumsindikiza Felix Tshisekedi na muungano wake katika udanganyifu mpya wa uchaguzi. Tunawakumbusha Wakongo kwamba kwa mujibu wa katiba, tuna wajibu wa kuzuia aina yoyote ya udikteta." Anasema mwanasiasa huyo ambaye uchaguzi uliopita alitazamiwa na wengi kushinda.


Kiongozi wa upinzani nchini DRC, Martin Fayulu.

### AIKOSOA TUME

Desemba mwaka jana, wapinzani Martin Fayulu, Augustin Matata Ponyo na mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel, mwaka 2018 Daktari Denis Mukwege, wanakosoa namna ambavyo tume ya uchaguzi CENI inavyoendesha shughuli za kuwasajili wapigakura.

> Pia, viongozi hao wanasema inaonekana dhahiri kwamba utawala uliopo, tayari umefanya mfumo wa udanganyifu mkubwa kwa uchaguzi huo.

Katika tangazo lao viongozi hao watatu wanasema kwa sasa DRC, inapitia mojawapo ya nyakati za giza zaidi tangu kuwepo kwake, wakiwataka raia wa DRC, kuamka na kuchukua majukumu yao kwa ujasiri na dhamira, ili wasiwe mashahidi na washirika wa ukandamizaji unaotokana na kutowajibika kwa serikali iliyopo.

Wanataka kuundwa upya kwa CENI na Mahakama ya Kikatiba na pia kusitishwa kwa zana zinazonyima haki wagombea urais.

Fayulu, Matata na Mukwege wanalaumu pia maandalizi ya mchakato wa kuandikisha wapiga kura wakisema mwanzo wa mchakato huo una hitilafu nyingi.

Akiwa mjini Kinshasa, Dieudonné Mushagalusa mwanaharakati wa shirika la kiraia aliyejaribu kupata kitambulisho cha mpigakura kutoka maeneo mbalimbali wanapoandikishwa bila kufaulu, anaeleza kuwa viongozi hao watatu hao Fayulu, Matata na Mukwege wanaona kwamba fursa hiyo ya uchaguzi ni muhimu.

Wanaamini ni muhimu kukomesha migogoro ya mara kwa mara iliyojitokeza nchini DRC, kuhusu uhalali wa matokeo ya uchaguzi, tangu uchaguzi wa mwaka 2006 kwa hiyo kuna haja ya kuuandaa inavyostahili.

Pia, viongozi hao wanasema inaonekana dhahiri kwamba utawala uliopo, tayari umefanya mfumo wa udanganyifu mkubwa kwa uchaguzi huo.

Upande wa chama tawala cha UDPS, wanachama wanasema huo ni woga tu na kuwataka waachane nao.

Martin Fayulu, Augustin Matata na Denis Mukwege wanataka pia usalama urejeshwe katika eneo la mashariki ya DRC na pia katika maeneo ya Maindombe na Kwilu, ili uchaguzi ufanyike huko katika hali tulivu.

Wanaahidi kuchukua jukumu la kutokubali uchakachuaji wowote ule wa matokeo ya upigaji kura wakati wa uchaguzi wa desemba mwakani na wanasema watahakikisha raia wa DRC, wanahamasihwa kuhusu hilo.

### FAYULU NI NANI?

Martin Fayulu ni mgombea mkuu wa upinzani katika uchaguzi wa urais DRC. NI miongoni mwa watu wenye ushawishi katika siasa nchini humo.

Mwaka 2018 vViongozi wakuu wa upinzani nchini DRC walimchagua mfanyabiashara huyo katika kinyang'anyiro cha uraisi, akichuana na mgombea mteule wa serikali, Emmanuel Ramazani Shadary ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani nchini humo.

Mgombea huyo ni mfanyabiashara mwenye umri wa miaka 61 ambaye mbali na kujihusisha na masuala ya kisiasa ni mwanasiasa maarufu nchini DRC, ambaye kati ya vitega uchumi vyake ni umiliki wa hoteli.

Alisoma nchini Marekani na Ufaransa lakini pia aliwahi kufanya kazi katika kampuni kubwa ya simu nchini Marekani na alikuwa mstari wa mbele katika kumfanyia kampeni ya kisiasa aliyekuwa kiongozi wa upinzani, marehemu Ettiene Tshisekedi.

Aidha, aliwahi kukamatwa mara kadhaa katika maandamano ya upinzani nchini DRC na wengi wameshangazwa na kuchaguliwa kwa Fayulu wanaomtazama kama mfanyabiashara kuliko kiongozi wa upinzani.

Wagombea wengine watakaoshiriki uchaguzi huo ni Felix Tshisekedi na Vital Kamerhe na kwamba uamuzi wa upinzani kuungana na kumchagua mgombea mmoja ni muhimu kwa sababu katika uchaguzi wa duru moja kuwapo wagombea wengi kutavunja hesabu ya uwingi wa upinzani na huenda ukaishia kushindwa.

Wakikutana kwa mara ya kwanza wote pamoja, viongozi hao wa upinzani pia wamekubaliana kuidhinisha mpango na kikosi cha pamoja na kampeni zinatarajiwa kuanza baadaye mwezi huu. **DW**

## 'Hazina ya taifa' inautaka uwakilishi bungeni, barazani

**INATOKA UK. 11**

### KUKWEPA WAZEE

Akimkaribisha Makamu wa Kwanza wa Rais, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma, anakemea mwenendo unaotumiwa na baadhi ya jamii kutelekeza wazee.

Riziki anasema baadhi ya watu wakiwamo vijana, wanatelekeza wazazi wao kwa kuwa serikali imejenga vituo vya kulelea wazee, hivyo wanakwepa majukumu yao na kuviachia vituo hivyo na kuwaonya:"Mtindo huo haukubaliki, serikali inajenga vituo si kwa lengo kutaka watoto wao wawasiwahudumie, bali ni kwa ajili ya wale wasio na ndugu au jamaa, lakini walionao wanapaswa kuwatunza."

Anasema, kwa sasa kuna vituo vitatu vya kulelea wazee hao ambavyo alivitaja kwa majina ya Sebuleni na Welezo vilivyopo Unguja na Limbani kilichopo Pemba, na kwamba vinawapatia wazee huduma muhimu ikiwamo chakula, malazi, mavazi matibabu na posho.

"Lakini jamii isikwepe majukumu ya kulea wazee na kuacha mtindo wa kuwapeleka katika vituo vya kulelea wazee. Hawa wanahitaji mapenzi, huruma kutoka kwa watoto wao na jamii inayowazunguka," anasema.

Anaongeza kuwa wazee ni hazina ya busara, halima na uzoefu ambavyo vyote ni muhimu kwa ustawi wa maisha, na kwamba ni lazima jamii na serikali iwe karibu nao kunufaika na tunu hizo kutoka kwao.

Waziri huyo anasema wizara yake inaendelea kujitahidi kufanya kila linalowezekana ili kutimiza ndoto za Rais wa Zanzibar za kutaka kuona wazee wanatunzwa na wanahudumiwa ipasavyo.





# Serikali kuboresha sera ya makazi ili kupunguza matatizo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amesema serikali ipo kwenye mchakato wa maboresho ya sera ya makazi ili kutoa suluhu ya matatizo yanayoikabili wizara hiyo, kuwashughulikia wasioendeleza maeneo yao.

Aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye mjadala wa kitaaluma wa kuadhimisha Siku ya Makazi Duniani unaolenga kujadili juu ya uchumi himilivu wa miji kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi.

"Mtu akipewa notisi anakwenda kuweka tofali mbili kwa kuwa hamna kanuni za uendelezaji, namna ya uendelezaji haujatajwa na sheria wala kanuni za uendelezaji wa ardhi hii inakwaza watu ambao wameendeleza na inaondoa dhana nzima ya makazi ya serikali,"alisema.

Alisema serikali inapopanga, kupima na kumilikisha ardhi ina nia ya kutengeneza makazi lakini na kukosesha serikali kodi ya majengo.

Alisema yatafanyika maboresho mengi ikiwamo mabadiliko ya michoro ya matumizi, upimaji na mipango miji, matumizi ya ardhi.

Silaa alisema ni muhimu kwenye mabadiliko ya matumizi ya ardhi yaangaliwe yana tija gani.

"Niwapongeze wizara kwa mfano eneo la Sinza tulikubaliana liwe la kibiashara na likabadilishwa matumizi, hivyo kama kuna mabadiliko ya ardhi yawanyike kwa eneo zima ili wananchi wajue," alisema.

Kuhusu mipango miji, alisema ni tatizo linalohitaji wizara ifanye mabadiliko makubwa na kupata muda wa kutafakari.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Anthony Sanga, alisema wizara hiyo ni ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi lakini kwa muda mrefu wamekuwa wakihangaika na migogoro ya ardhi.

Alisema: "Tumefanya mengi kuhusu maendeleo ya makazi lakini hatujafanya vizuri sana na ndiyo maana bado ujenzi holela unaendelea maeneo mbalimbali, pamoja na kazi kubwa inayofanyika ya urasimishaji lakini bado kuna changamoto".

# Ajali 1,720 zasababisha vifo vya watu 1,545 mwaka 2022

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi imesema mwaka 2022 ajali 1,720 zilitokea na kusababisha vifo vya watu 1,545, huku watu 2,278 wakijeruhiwa.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Jumanne Sagini, aliyasema hayo jana katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Huduma kwa Wakimbizi, Kamishna wa Polisi, Nsato Marijani.

Takwimu hizo zilitolewa wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Kuwa salama barabarani Afrika' inayolenga kuboresha usalama wa watoto barabarani.

Kampeni hiyo imeanzishwa kwa ushirikiano wa Kampuni ya Puma Energy kwa kushirikiana na Amend Tanzania yenye lengo la kuleta mabadiliko ya usalama barabarani, ili kuwawezesha watoto na kuboresha usalama wao na vijana barabarani nchini.

"Majeraha ya ajali za barabarani ndiyo chanzo kikuu cha vifo vya watoto na vijana kote ulimwenguni, huku Afrika ikiwa na viwango vya juu vya vifo vya barabarani. Na takwimu za Jeshi la Polisi za mwaka 2022 zinaonesha idadi hiyo ya ajali, vifo na majeruhi na watoto wakiwa katika hatari kubwa," alisema Sagini.

Hivyo, alipongeza kuanzishwa kwa kampeni hiyo na kuchaguliwa shule tano zilizoko katika maeneo ya hatari ambazo ni Shule ya Msingi Kibugumo, Shule ya Msingi Kifuru, Shule ya Msingi Msewe, Shule ya Msingi Kibasila na Shule ya Msingi Mtambani.

Alisema hatua zilizochukuliwa na serikali kuboresha miundombinu ya barabara zimelenga kuwafanya wamiliki, madereva, abiria na watumiaji wa barabara kuwa na matumizi yenye ufanisi na siyo kuwa chanzo cha ajali.

Sagini alisema kupitia kampeni hiyo itakayotekelezwa na Amend Tanzania, itawapa watoto wa shule za msingi maarifa na ujuzi muhimu wa usalama barabarani.

Alitaja shughuli hizo kuwa ni pamoja na kuchora na 'mahakama ya watoto' ambayo huwawezesha watoto na watu wazima kwa kuendesha gari kwa uzembe karibu na shule zao.

Naye Meneja Mkuu wa Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah, alisema kila mtoto anastahili safari salama ya kwenda shule na kurudi.

Alisema mpango huo tangu aunze uliwanufaisha zaidi ya watoto 130,000 katika shule zipatazo 115 nchini katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Mbeya, Mwanza, Ruvuma na Zanzibar.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Amend inayoshughulikia masuala ya usalama barabarani, Saimon Kalolo alisema Puma Energy na Amend wamekuwa kwenye mpango wa usalama barabarani tangu mwaka 2013 wakitekeleza katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar. Alisema kampeni hiyo iliyozinduliwa itatekelezwa Dar es Salaam katika shule hizo tano na nchi nyingine za Zambia, Zimbabwe na Botswana.

Ofisa Mnadhimu wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna Msaidizi Pili Misungwi, alitaja makosa yanayosababisha ajali barabarani na kusababisha vifo, uharibifu wa miundombinu na majeruhi kuwa ni matumizi ya vilevi au dawa za kulevya, mwendokasi, uzembe wa kutotii sheria za barabarani na matatizo ya kiufundi ya chombo cha moto.




Meneja Msimamizi wa Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), George Nyamrunda (kushoto), akichangia mada katika kongamano la saba la uwezeshaji wananchi kiuchumi jijini Dodoma jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, Fatma Kange. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC abaini wizi vifaa vya ujenzi katika shule ya sekondari

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amebaini uwapo wa wizi wa vifaa vya ujenzi katika shule ya sekondari wasichana mkoani hapo, inayojengwa katika Kata ya Manchali wilayani Chamwino na kuagiza wahusika wachukuliwe hatua kali.

Alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifanya mazungumzo na kutoa maelekezo kwa mafundi wanaotekeleza ujenzi huo wa shule hiyo.

"Hapa jana imekamatwa mifuko 10 ya saruji iliyokuwa imebebwa na bodaboda wawili kila mmoja mitano lakini hatujui ilikusudiwa mingapi kuchukuliwa. Hapa kwetu sisi haijalishi ni mfuko mmoja au mitano au 100 kwetu sisi inathamani kwa sababu itasababisha kuharibika kwa ubora wa kazi kwa kile ambacho kimekusudiwa," alisema.

Hivyo, aliagiza hatua kali zichukuliwe kwa wote wanahusika na wizi huo ili iwe fundisho kwa wengine.

"Sasa nitoe agizo kwa kuwa na pamoja wahalifu wameshikwa tupate taarifa ya hatua zilizochukuliwa kwa wote waliohusika haijalishi awe na cheo gani hakikisheni wanachukuliwa hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine," aliagiza.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya alimhakikishia Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kuwa atatekeleza maagizo yake ya kuwachukulia hatua kisheria.

Awali, Ofisa Tarafa wa Chilonwa, Japhari Kikoti, alisema halmashauri itahakikisha inakamilisha mradi huo bila kusuasua, kwamba shule hiyo inajengwa kwa Sh. bilioni tatu na itakamilika mwishoni mwa mwaka huu.

# Malalamiko walimu kutolipwa posho, serikali yatoa agizo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na kuwapo na malalamiko ya baadhi ya walimu wapya kutolipwa fedha za kujikimu, serikali imewaagiza maofisa elimu wa mikoa na wilaya kufuatilia na kuhakikisha wanapata fedha zao kwa wakati.

Agizo hilo limetolewa na Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, wakati wa kikao kazi cha maofisa elimu, kusema takwimu zinazopelekwa wizarani zinaonyesha walimu hao wamelipwa lakini bado kuna malalamiko.

"Niwaagize hakikisheni mnalifanyia kazi hili kwa kuangalia wote wanaostahili kulipwa na bado hawajalipwa fedha hizo ziweze kulipwa mara moja, pia hakikisheni mnakwenda kusikiliza na kutatua kero zilizopo ndani ya uwezo wenu," alisema.

Kadhalika alisema TAMISEMI itafanya tathmini na kuchukua hatua stahiki kwa wasimamizi watakaobainika kufanya uzembe katika usimamizi na ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa shule mpya kupitia mradi wa BOOST na SEQUIP.

Ndejembi alisema kuanzia sasa serikali haitamvumilia kiongozi yeyote ambaye hatatimiza majukumu yake kikamilifu hasa katika suala zima la usimamizi wa miradi.

Aliwahimiza viongozi hao kuhakikisha miradi yote ya ujenzi wa shule mpya na miundombinu ya shule za msingi na sekondari inakamilika kwa wakati na kwa kuzingatia ubora na thamani ya fedha.

"Shule zote mpya ziwe zimesajiliwa tayari kwa kupokea wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kabla au ifikapo Oktoba 30 mwaka huu," alisema.

Pia aliwahimiza kusimamia kikamilifu ufundishaji na ujifunzaji katika shule za msingi na sekondari ili kuhakikisha wanafunzi wote wa darasa la kwanza na pili wanamudu stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).

Aidha, aliwaagiza uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali na darasa la kwanza uanze mara moja Oktoba Mosi hadi Desemba 31 mwaka huu, ili shule zinapozinduliwa Januari mwakani wanafunzi wote waanze masomo mara moja.

Pia alisisitiza kuimarishwa kwa mifumo ya usimamizi wa ulinzi na usalama wa wanafunzi ili kuzuia na kubaini matukio ya ukatili na unyanyasaji kwa wanafunzi.





# Wabunge wataja chanzo mazao kuuzwa bei chee

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WABUNGE wa Rungwe na Busokelo pamoja wa Viti Maalum mkoani Mbeya, wamesema mazao ya wananchi wilayani Rungwe yanauzwa kwa bei ndogo kutokana na ubovu wa barabara unaosababisha yashindwe kufika sokoni kwa wakati.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Kandete katika Halmashauri ya Busokelo na kuhudhuriwa na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba.

Walisema ujenzi wa Barabara ya Katumba - Lupaso yenye urefu wa kilomita 35 ambao umeanza utasaidia kupandisha bei ya mazao mbalimbali ambayo wananchi wanazalisha katika maeneo hayo.

Barabara hiyo ni sehemu ya Barabara ya Katumba - Lwangwa - Mbambo -Tukuyu yenye urefu wa Km. 80 ambayo inaunganisha Halmashauri ya Rungwe na Busokelo.

Mbunge wa Busokelo, Atupele Mwakibete, alisema wananchi wa Busokelo wanazalisha kwa wingi ndizi, chai, maparachichi na kakao lakini mazao hayo kwa muda mrefu yamekuwa yakiuzwa kwa bei ndogo kutokana na ukosefu wa miundombinu mizuri ya barabara.

Alisema mbali na uzalishaji wa mazao hayo, pia katika jimbo lake kuna uzalishaji wa maziwa, kiwanda cha gesi, kiwanda cha chai, bidhaa ambazo zinahitaji uwepo wa barabara nzuri ili bidhaa hizo zifikishwe sokoni haraka na kuwanufaisha wananchi.

"Licha ya wananchi wetu kufanya kazi kubwa na nzuri kwenye uzalishaji wa mazao haya, bado mazao haya hajawanufaisha kutokana na ubovu wa barabara, hivyo tunaamini endapo barabara hii itajengwa itakuwa ni mkombozi mkubwa wa uchumi kwa wananchi wetu," alisema Mwakibete.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakiomba serikali kuwajengea barabara hiyo bila mafanikio lakini sasa wameanza kuona mwanga.

Alisema barabara hiyo mbali na kusafirisha mazao pia itasaidia huduma za kijamii kuwafikia wananchi kirahisi katika maeneo hayo na hivyo kuwezesha shughuli za maendeleo kusonga mbele kwa kasi.

"Sisi kama wabunge kwa muda mrefu tumekuwa tukipiga kelele bungeni kuomba barabara hii ijengwe, tunashukuru kelele zetu sasa zimesikika na serikali sasa imeamua kuijenga, huu ni uamuzi sahihi kwa kusaidia maendeleo ya wananchi wetu," alisema Mwakagenda.

Mwakagenda alisema chama chake kitaendelea kufanya kazi ya kuikumbusha serikali kutekeleza miradi ya kuwanufaisha wananchi ikiwamo ujenzi wa barabara hizo.

Kwa upande wake Suma Fyandomo ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya kupitia CCM, alisema kuwa uamuzi wa serikali kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami utasaidia kuboresha huduma za kijamii kwa wanawake.

Alisema wanawake wamekuwa wakipata shida kusafiri kwenda kupata huduma za afya katika hospitali ya wilaya lakini baada ya barabara hiyo kukamilika watakuwa wanasafiri kirahisi.

Waziri wa Ujenzi, Bashungwa aliagiza Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) Mkoa wa Mbeya kuifanyia upembuzi Barabara ya Kandete - Makete kupitia safu za Milima ya Livingistoni yenye urefu wa Kilomita tisa ambayo ilianza kulimwa na wananchi kwa majembe ya mkono ili iwekwe kwenye vipaombele vya wizara.

Alisema barabara hiyo itatumika kwa ajili ya kupunguza magari katikati ya Jiji la Mbeya kwa maelezo kuwa magari yote yanayotoka Kyela na Rungwe kwenda Dar es Salaam na Dodoma yatakuwa yanapitia huko.

## Shule yakabiliwa na upungufu wa walimu wa kike

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

SHULE ya Sekondari ya Kanga iliyopo katika Wilaya ya Songwe inadaiwa kuwa na walimu wawili pekee wa kike, huku ikiwa na zaidi ya wanafunzi 400 wa jinsi hiyo hali inayowafanya waelemewe wakati wa kuwahudumia.

Mkuu wa shule hiyo, Mwalimu Leonard Mpoli aliyasema hayo wakati wa ziara ya Mbunge wa Viti Maalumu wa Mkoa wa Songwe, Neema Mwandabila ambaye aliambatana na madiwani wa Viti Maalumu wa Wilaya ya Songwe kwenye ukaguzi wa miradi.

Alisema shule hiyo ina zaidi ya wanafunzi 800 na walimu 24 lakini wa kike ni wawili pekee ambao wanashindwa kuwahudumia wanafunzi wa kike kwa ufasaha.

Alisema kwa idadi ya wanafunzi wa kike iliyopo shuleni hapo walitakiwa kuwa na walimu wa kike zaidi ya 10 ili angalau wawe na uwezo wa kuwahudumia wanafunzi hao.

"Kuna mambo ya wanafunzi wa kike ambayo hawawezi kutueleza sisi walimu wao wa kiume, kwa hiyo kitendo cha idadi ya walimu wa kike kuwa ndogo kinasababisha washindwe kuwahudumia vizuri," alisema Mwalimu Mpoli.

Hivyo, aliiomba serikali kuwaongezea walimu wa jinsi hiyo ili wawahudumie vizuri wanafunzi wa kike.

Diwani Viti Maalum, Paskalia Shitundu, alisema wanafunzi wa kike wana matatizo mengi ambayo hawawezi kumwambia mwalimu wa kiume, hivyo serikali iangalie namna ya kuongeza walimu wa kike shuleni hapo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Songwe, Philip Malika, alisema kutokana na tatizo hilo watahakikisha kwenye mgawo wa walimu wanazingatia usawa wa kijinsia hasa kwa kuongeza walimu wa kike kwenye shule hiyo.

Akizungumza na walimu pamoja na wanafunzi wa shule hiyo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe, Neema aliipongeza serikali kwa kujenga miundombinu bora shuleni akisema atahakikisha anapigania ili walimu wa kike waongezwe.




Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja wa Tigo, Mwangaza Matotola (kushoto) na Mkurugenzi wa Tigo Nyanda za Juu Kusini, Abas Abdulrahman, wakipeperusha bendera kuashiria uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja mkoani Iringa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuongeza miundombinu ya TEHAMA shuleni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

SERIKALI mkoani Njombe imesema imejipanga kuongeza miundombinu ya TEHAMA kwenye taasisi za elimu hasa shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi pamoja na kuongeza ufaulu.

Kauli hiyo ilitolewa na Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari, wakati akifunga mafunzo ya walimu wakuu wa shule za msingi mkoani hapa yaliyofanyika katika Chuo cha Walimu Tandala wilayani Makete na kusimamiwa na Wakala wa Maendeleo ya Elimu ya Uongozi (ADEM).

Pia alisema shule za msingi mkoani Njombe zinatakiwa kujiendeleza katika matumizi ya TEHAMA ili kuamsha ari na kupiga hatua katika ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi shuleni.

"Suala la kuweka TEHAMA katika usimamizi, uongozi na ufundishaji shuleni ni kipaumbele chetu kama mkoa na kwenye hili tunashirikiana na halmashauri na Wizara ya Elimu kutafuta njia bora za kufundisha na kujifunzia," alisema Omari.

Alisema kutokana na maboresho kwenye sekta ya elimu kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi na kukabiliana nalo, serikali imeboresha miundombinu mipya ya shule.

Naibu Mtendaji Mkuu, Mipango, Fedha na Utawala (ADEM), Dk. Emmanuel Mollel, alisema kupitia mafunzo waliyopata walimu hao wakuu hawategemei kuona taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) inatokea matatizo kwenye mahesabu yao ya shule.

Mratibu wa mafunzo ya walimu katika Kituo cha Chuo cha Ualimu Tandala, Janeth Mwanjejele, alisema walimu wakuu walioshiriki mafunzo hayo mkoani Njombe ni 516 ambapo awamu ya kwanza walikuwa walimu 260 na awamu ya pili 256.

Alisema walimu hao wamejengewa uwezo katika maeneo ya uongozi, usimamizi na uendeshaji wa shule, utawala bora wa elimu, uendeshaji wa ofisi.

Pia walifundishwa utunzaji wa kumbukumbu shuleni, ukusanyaji wa takwimu na uaandaji wa mpango wa jumla wa maendeleo ya shule.

"Walimu hawa pia wameweza kujifunza namna ya ushirikishwaji wa jamii na namna ya kushughulikia malalamiko yanayoweza kujitokeza shuleni," alisema Mwanjejele.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Watson Anyisile alishukuru serikali kuwakumbuka walimu wakuu nchini na kuwapatia mafunzo hayo yanayokwenda kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.



## Ushirikiano Tanzania, nchi za Afrika unaleta umoja rasilimali za baharini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame amesema ushirikiano kati ya Tanzania na nchi Afrika unaleta umoja wa kutumia rasilimali za baharini, ili kupata maendeleo katika kuijenga Afrika.

Aliyasema hayo visiwani Zanzibar wakati akifungua mafunzo ya siku moja ya maofisa wa Jeshi kutoka nchi ya Malawi, Msumbiji, Zambia, Kenya na Tanzania yaliyohusu matumizi ya teknolojia na usalama wa bahari katika uchumi wa buluu Afrika.

Alisema ushirikiano baina maofisa wa kijeshi wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) kwa ajili ya kujifunza uchumi wa buluu kutaongeza nguvu ya pamoja ya undugu hasa katika kupambana na uhalifu wa baharini, uvuvi haramu, pamoja na kuhifadhi mazingira.

Naye, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Aboud Suleiman Jumbe alisema ujio wa maofisa hao wa kijeshi kufika Zanzibar kujifunza masuala ya uchumi wa buluu kunaongeza zaidi ushirikiano wa ulinzi na usalama wa baharini katika Kanda ya Magharibi ya Bahari ya Hindi.

Alisema, Tanzania inaushirikiano mzuri na nchi mbalimbali za Afrika katika matumizi sahihi ya rasilimali za baharini ili kuleta manufaa kwa nchi wanachama za ukanda wa bahari wa Afrika.

Akizungumza baada ya mafunzo hayo, Kanali Lauran Lugenge, kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), alisema kuwa mafunzo hayo yamesaidia katika kujifunza namna ya matumizi sahihi ya bahari, lakini pia kwa namna gani bahari inawainua wananchi kiuchumi kupitia uchumi wa buluu.

# Nyani wageuka kero Kisiwa cha Tumbatu, wakulima walia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKULIMA wa Kisiwa cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja, wameiomba serikali kuwatokomeza wadudu waharibifu wa mazao yao ikiwemo kima (nyani) ambao ni wengi katika kisiwa hicho.

Wakizungumza katika kikao cha kuwasilisha kero na changamoto zinazowakabili kati ya wananchi na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, wakulima hao walisema idadi ya kima ni wengi kuliko idadi ya wakazi wa kisiwa hicho.

Haji Muhammed Haji, miongoni mwa wakulima hao, alisema kima hao wanakula mazao yao hali ambayo inarejesha nyuma juhudi zao za kuendelea na kilimo.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kima ni wengi kuliko sisi wananchi wa kisiwa hiki cha Tumbatu, tumeshawachoka, tunaomba msaada wenu wa kuwaangamiza kima hawa maana wanatuweka na njaa" alisema mkulima huyo.

Aidha, alisema kilimo kikuu wanacholima kisiwani humo ni choroko, kunde, mahindi, mbaazi na mihogo kwa sababu ardhi yao ni ya jiwe licha ya kuzungukwa na bahari.

Alisema kwa sasa hali ni tete njaa zimetawala kutokana na wanyama hao waharibifu na hawana nyenzo za kuwazibiti.

Mtumwa Ngwali Haji, alisema wanyama hao huwafanyia visa wakulima wanawake wanapokuwa mashambani na hawana hofu yoyote wanapowaona ikilinganishwa na wakulima wanaume.

"Wanapotuona sisi wakulima wanawake hutufanya kama shoga zao, wanapotuona hutufanyia visa haswa kwa kweli tumeshawachoka hatutaki hata kuwaona" alisema.

Akizungumzia tatizo hilo la kima, Katibu Tawala wa Kisiwa hicho, Khatib Habibu alikiri uwepo wa idadi kubwa ya kima katika kisiwa hicho ikilinganishwa na idadi ya wakazi ambapo kisiwa hicho kina idadi ya wananchi 11,955 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Alisema, tatizo hilo lipo kwa muda mrefu lakini kwa sasa limezidi kushika kasi kwa sababu wanyama hao wanaendelea kuzaliana na kuharibu mazao ya wakulima.

Alisema wananchi wa kisiwa hicho wamehamasika na kilimo lakini hawana wanachokivuna kwa sababu ya kima kuhujumu mazao kabla ya muda wa kuvunwa kufika.

"Miaka ya nyuma tulikuwa na zoezi la kuangamiza kima katika kisiwa chetu lakini kwa sasa zoezi hili limesitishwa kwa sababu linahitaji gharama"alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Ayoub Mahmoud, alisema serikali ya mkoa wake inatarajia kufanya utafiti kuhusu wanyama hao hawaribifu kijiji hapo na kutafuta njia za kuwaangamiza ili wakulima kunufaika na kilimo. Alisema ili kuwaangamiza wanyama hao kunahitajika gharama ya Sh. milioni tano kwa ajili ya kununua marisasi ya kuwapiga na kuwaua wanyama hao pamoja na gharama zingine na Serikali ya Mkoa inafanya juhudi ya kutafuta fedha hizo.

Hivyo, aliwataka wakulima kuendelea kuwa wavumilivu wakati serikali inafanya juhudi za kutatua changamoto hiyo, ili wakulima kunufaika na kilimo lakini pia kupata chakula na kuondokana na njaa.

Kisiwa cha Tumbatu ni miongoni mwa visiwa vidogo nane vya Unguja na Pemba na serikali imefikisha huduma mbalimbali muhimu ikiwemo, miundombinu ya afya, elimu, maji na umeme.

Kisiwa hicho nyenye shehia nne ikiwemo Jongowe, Gomani, Uvivini na Mtakuja kina wananchi 11,955 lakini idadi ya kima waliopo ni zaidi ya idadi hiyo ya wananchi.

Kima wanaopatikana katika kisiwa hicho ni kima punju ambao wanapatikana katika Msitu wa Hifadhi ya Jozani na ni kivutio kikubwa cha watalii, bali kima aliopo Tumbatu ni weusi ambao ni adui kwa mazao ya kilimo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman (kushoto), akizungumza na uongozi wa Taasisi ya Mpango wa Hiyari wa Tathmini ya Utawala Bora Barani Afrika (APRM - Tanzania), ofisini kwake Mazizini nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali: Tumefanikiwa kutekeleza dhana ya utawala bora

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema serikali imejipanga kutekeleza dhana ya utawala bora katika kudhibiti mapato pamoja na kuweka wazi taarifa za ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kusomwa hadharani.

Aliyasema hayo jana ofisi kwake Mazizini Mjini Zanzibar, alipokutana na uongozi wa Taasisi ya Mpango wa Hiari wa nchi za Umoja wa Afrika Kujipima katika vigezo vya Utawala Bora (APRM) Tanzania.

Timu hiyo iliongozwa na Katibu Mtendaji wa APRM Tanzania, Lamau Mpolo, Mratibu wa Eneo la Uchumi Jamii, Balozi Hemed Mgaza pamoja na Meneja wa Mawasiliano, Badria Masoud Atai.

Waziri huyo alisema katika kipindi cha miaka miwili na nusu ya uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi mafanikio makubwa yamefikiwa katika utekelezaji wa dhana ya utawala bora katika matumizi ya fedha, hatua ambayo imesaidia kukuza uchumi na ukuaji wa pato la taifa.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili ripoti zote za CAG zinasomwa hadharani, hatua ambayo imewawezesha watendaji wa serikali na wananchi kujua kasoro na matukio ya ubadhirifu wa fedha za serikali.

Aidha, alisema zipo kamati katika Baraza la Wawakilishi zikifuatilia kwa karibu ripoti ya CAG kwa ajili ya kuifuatilia kujua kasoro za utendaji na viongozi wa serikali katika masuala ya matumizi mabaya ya fedha.

Aliyataja baadhi ya maeneo ambayo yamefanyiwa maboresho makubwa ni pamoja na taasisi zinazosimamia haki ikiwemo Mahakama.

Alisema maboresho hayo matunda yake yameonekana ikiwemo kesi mbalimbali za wananchi kusikilizwa kwa haraka na kutolewa maamuzi yake, hatua ambayo imepunguza malalamiko kwa wananchi.

Waziri huyo alisema serikali imeunda idara ya utawala bora kwa ajili ya kufuatilia kwa karibu matukio yote yanayokwenda sambamba na kulinda haki za binaadamu.

Katibu Mtendaji wa APRM Tanzania, Lamau Mpolo, alisema uongozi wa APRM umefika katika wizara hiyo kwa ajili ya kujitambulisha.

Lamau alisema kuwa malengo na madhumuni ya APRM ni kukuza dhana ya utawala bora kwa kuzingatia vigezo vinavyokubalika kimataifa, hivyo itahakikisha misingi yake inazingatia na kufikia viwango vya kimataifa.

Alisema mpango wa APRM utahakikisha ripoti inayotayarishwa inafikia vigezo vya kimataifa na kuweza kuharakisha shughuli za kimaendeleo pamoja na kuimarisha muungano wa kikanda na Afrika.

# TCRA yaja na mfumo wateja kutoa maoni

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inatarajia kuanzisha mfumo wa kisasa utakaojulikana kwa jina la Tanzanite Portal, utakaotoa fursa kwa wateja wake kutoa maoni.

Mkurugenzi wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alibainisha hayo jana alipotembelea dawati la wateja na kushirikiana na wafanyakazi wengine wa mamlaka hiyo kutoa huduma kwa wateja katika Wiki ya Huduma kwa Wateja.

Alisema kuanzishwa mfumo huo kutasaidia kuimarisha mazingira bora ya huduma kwa wateja na walaji na kuleta mapinduzi katika utoaji huduma za mawasiliano nchini.

Pia alisema kuanzishwa kwa mfumo huo kutasaidia kupunguza urasimu katika utoaji leseni za mawasiliano.

"Mawasiliano ni uhai wa taifa letu na tuna wajibu wa kuhakikisha yanafanyika bila vikwazo kwa manufaa ya Watanzania wote. Na kwa hili tumejipanga ili itusaidie kutoa huduma ya kipekee kwa wadau wetu hususani watumiaji na wateja wa huduma za mawasiliano.

"Tunataka kuhakikisha mtoa huduma anatimiza wajibu wake kwa ufanisi. Tanzanite Portal ambayo inapatikana kupitia tovuti ya mdhibiti wa mawasiliano, imeundwa ili kurahisisha mawasiliano kati ya TCRA na watoa huduma wote wa sekta ya hii, siyo tu kusikiliza kero zao bali pia kuchukua hatua madhubuti na kuzishughulikia," alisema.

Dk. Bakari alisisitiza kuzingatia umuhimu wa kurekodi na kuchambua maoni yanayopokewa kutoka kwa watumiaji na kwamba hiyo ni moja ya mbinu ya kusaidia katika uboreshaji wa sera pamoja na mipango ya kuimarisha zaidi sekta ya mawasiliano nchini.



"Takwimu tunazokusanya kutoka kwa wadau wetu zitaleta mabadiliko chanya na kwa kuwa dhamira yetu ni thabiti, kwa kushirikiana na wateja wetu, Tanzania itaendelea kufurahia huduma za kisasa za mawasiliano," alisema Dk. Jabiri.

Miongoni mwa wateja waliopewa huduma na mkurugenzi huyo wa TCRA ni Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa Airtel, Beatrice Singano ambaye pamoja na mambo mengine, alipongeza maboresho yanayofanywa na mamlaka hiyo hadi sasa katika kuhudumia wadau wake.

"Nimefurahishwa na jinsi mdhibiti wetu anavyofanya kazi zake kwa sasa hususani kwenye dawati la wateja ni nzuri sana, rafiki, na ninaamini ujio wa Tanzanite Portal ni mwanzo mwingine mzuri zaidi katika utoaji wa huduma za mawasiliano nchini," alisema Singano.

Eugenia Chanda, mdau wa mawasiliano kutoka Dar es Salaam, alisema kuanzishwa kwa mfumo wa kisasa wa wateja kutoa maoni ni hatua nyingine ya maendeleo inayofanywa na TCRA. Anaamini itasaidia kuongeza ufanisi na uwazi katika utoaji huduma hiyo nchini.


IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

Probate and Administration Cause No 107 of 2023

In the Matter of the Estate of the LATE GAUDENCIA BENEDICT MAGAGA Of Kikuyu within Dodoma City

And

In the matter of application for letters of administration by THERESIA LAWRENCE MAGAGA

GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 11 day of 10........................ 2023
Dated at Dodoma this 20 day of 09..................2023

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE
Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM
Usimamizi wa Mirathi Na. 1456/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU SHELA MAULID WA KARENGA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA
MSIMAMIZI YALIYOLETWA
NA KASHINDI MAULID KARENGA
TANGAZO
(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 mwezi 10 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetokewa leo tarehe 25 mwezi 09 mwaka 2023.

HAKIMU

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

INOSENT FRANK CHAMI anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 496 DFT aina ya HIACE . Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi :PHQ/DOD/DOD/4368/2023

IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
(TANGA DISTRICT REGISTRY)
AT TANGA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 5 OF 2023

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DR. MACHAGE MASARU WABEYA

AND

IN THE MATTER OF APPLICATION FOR PROBATE BY KUNG'E NYAMHANGA WABEYA AND IMANI MACHAGE WABEYA

GENERAL CITATION
(Made Under Rule 75 of the Probate Rule)

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioners.

The Petition has been fixed for Hearing on 23rd Day of October, 2023 before Hon. H.P Ndesamburo J.
Objections to the grant should be filed on or before the 23rd day of October, 2023.

Dated at Tanga this 02th Day of October, 2023.

Deputy Registrar
TANGA

KUPOTEA KWA CHETI



**HAMSINI BAKARI SHABAAN,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha NNE chenye Index no **S.4779.0018** Kilichotolewa na baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya sekondari ILINDI Mwaka 2020 Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/BAH/2506/2023**

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BERNARD MERERE MWANGANYA,** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI LENYE NAMBA ZA USAJILI **T. 291 EAC,** ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI **PHQ/MBE/3196/2023.**




Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, akiongoza Menejimenti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kukagua ujenzi wa jengo la ofisi hiyo unaoendelea katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Washikiliwa kwa tuhuma kukutwa na noti bandia

**Na Moses Ng'wat,** SONGWE

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe linawashikilia wanaume wawili, akiwamo raia wa Zambia kwa tuhuma za kukutwa na noti bandia na karatasi za kuchapisha noti bandia kwa lengo la kujipatia kipato kwa utapeli.

Watu hao na wenzao ambao wanatafutwa na jeshi hilo kwa madai ya kuunda mtandao wa kutengeneza noti katika mpaka wa Tunduma, pia wanadaiwa kukutwa na vitambulisho vya taifa vya nchi ya Zambia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Theopista Mallya, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema watuhumiwa hao walikamatwa Septemba 19 mwaka huu katika Mtaa wa Mwaka Kati, mjini Tunduma, wilayani Momba.

Kamanda Mallya licha ya kutowataja majina watuhumiwa hao kutokana na sababu maalum za kipolisi, alisema watuhumiwa hao akiwamo raia huyo wa Zambia ambaye ni mkazi wa Mpulingu (Zambia), walikutwa na noti bandia 12 ambazo ni fedha za Zambia zikiwa zimechapishwa kwa thamani ya Kwacha 50.

Alisema watuhumiwa hao pia walikutwa na karatasi 10 zenye ukubwa wa A4 zikiwa zimechapishwa kama Kwacha 50 kwa idadi ya noti 36, pamoja na karatasi nyingine moja iliyochapishwa noti nne zenye thamani ya Kwacha 100 zikiwa na namba EJ.228951989 na EJ.17714847.

"Lengo la watuhumiwa kufanya matukio haya ni kujipatia kipato isivyo halali na mbinu iliyotumika ni kutengeneza noti bandia kwa kutumia kompyuta, printa na karatasi za A4," alifafanua Kamanda Mallya.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa na visu viwili vikubwa na kidogo cha kukunja, mkasi mmoja wa kukatia karatasi pamoja na vitambulisho vya taifa vya Zambia.

## HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# Moto Kariakoo waibua mapya

**Na Restuta James**

SERIKALI imeagiza mikoa, wilaya na halmashauri zote za miji kufanya tathmini ya uwezo wake kukabili majanga hasa ya moto na kuweka mikakati ya kuyakabili.

Pia imeagiza mamlaka hizo kufanya kazi kwa karibu na mamlaka za maji ili kuweka maeneo maalum ya magari ya zimamoto kuchukua maji pindi linapotokea janga la moto.

Ni maagizo yaliyotolewa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deo Ndejembi, alipotembelea soko la Kampuni ya Kariakoo Auction Mart lililoteketea kwa moto Jumapili iliyopita.

Akimwakilisha Waziri Mohamed Mchengerwa, naibu waziri huyo alisema: "Mheshimiwa Mchengerwa ameniagiza kuelekeza wakuu wote wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha wanafanya tathmini katika maeneo yao ya utawala ya utayari wa kukabiliana na majanga kama haya ya moto kama hapa Dar es Salaam na hapa Kariakoo kuhakikisha wanashirikiana na mamlaka ya maji kuwa na maeneo kwa ajili ya maji ambayo zimamoto wanaweza kuyatumia.

Ndejembi alisema tathmini hiyo inatakiwa kuanza mara moja ili kujihakikishia uwezo wa kukabili majanga na kupunguza hasara kwa wananchi.

Alisema lengo la ziara yake sokoni huko ni kuona namna ambavyo serikali itaboresha uwezo wake wa kudhibiti majanga yanapotokea.

Ndejembi pia alisema wanasubiri taarifa ya kamati iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuchunguza chanzo cha moto huo ili serikali ichukue hatua stahiki.

Alisema maoni na mapendekezo ya timu hiyo yatafanyiwa kazi haraka ili kuleta utulivu kwa wananchi na wafanyabiashara.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alisema chanzo cha moto hakijajulikana na kuwataka wafanyabiashara kuendelea kuwa watulivu wakati serikali inasubiri ripoti ya uchunguzi.

Alisema timu hiyo imepewa siku saba kukamilisha kazi hiyo na utekelezaji wa mapendekezo utafanyika mapema.

Mwenyeketi wa soko hilo, Salehe Msoka, aliishukuru serikali kwa namna ambavyo viongozi wa mkoa na wilaya walisaidia kudhibiti janga hilo.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Kariakoo, Martin Mbwana, alisema wako tayari kushirikiana na serikali huku akiwataka wafanyabiashara kuwasilisha maoni na mapendekezo yao kwa timu ya Mkuu wa Mkoa na itakayoundwa kufanya tathmini.

Baadhi ya wafanyabiashara walimwomba Ndejembi kuwapo utaratibu wa serikali kuwashirikisha inapounda timu za tathmini ya hasara.

Moto huo ulioathiri zaidi ya wafanyabiashara 500, ulizuka Jumapili Oktoba Mosi saa 12:30 asubuhi kwenye soko la Kampuni ya Kariakoo Auction Mart.

## Ruto 'abariki' wanajeshi wake 1,000 kwenda Haiti

**Nairobi,** KENYA

RAIS wa Kenya, William Ruto, ameafiki idhini ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kupelekwa kwa maofisa usalma wa Kenya Haiti.

Baraza hilo lenye wanachama 15, siku ya Jumatatu lilipitisha azimio linaloidhinisha ujumbe wa 'Kikosi cha Usaidizi wa Usalama wa Kimataifa' unaoongozwa na Kenya, kwa ajili ya kuwasaidia polisi wa Haiti, kupambana na magenge ya uhalifu.

Azimio hilo lililoandaliwa na Marekani na Ecuador, liliidhinishwa kwa kura 13 za Ndio huku China na Russia, zikijizuia kupiga kura.

Kupitia taarifa kwa vyombo vya habari, Rais Ruto aliafiki uamuzi wa baraza hilo, akiutaja kuwa chombo muhimu cha kufafanua ujumbe wa kimataifa.

Ruto, alielezea ujumbe huo kama wajibu wa kimaadili kwa jumuiya ya kimataifa.

"Hali ya Haiti ni suala la kuzingatia kibinadamu, uwajibikaji wa kimaadili na haki ya kimsingi, hatua zinapaswa kuongezwa kwa kiasi kikubwa, ili kukidhi mahitaji ya misaada ya dharura, misaada ya kibinadamu.

"Msaada wa maisha na uingiliaji kati mkubwa katika afya ya umma na ulinzi wa mazingira," alisema.

Kenya, inatarajiwa kuwapelekea maofisa wake wa usalama nchini Haiti, huku kukiwa na ghasia za magenge ambayo yametikisa mji mkuu wa nchi hiyo ya Caribbean Port-au-Prince, kwa zaidi ya mwaka mmoja. Imejitolea kutuma wanajeshi 1,000 nchini Haiti, huku Bahamas wakiwa wamejitolea kuwapeleka wanajeshi wake 150 huku Jamaica, Antigua na Barbuda, zikiahidi kusaidiana. **BBC**




Kamishna wa Polisi, Nsato Marijani (wa nne kushoto), akiwa pamoja na washiriki baada ya kuzindua Programu ya Elimu ya Usalama Barabarani ya 'Be Road Safe Afrika' inayotekelezwa na Kampuni ya Puma Energy Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Puma Energy, Selemani Magige (wa sita kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Fatma Abdallah (mwenye ushungi), Mnadhimu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, ACP Pili Misungwi (kushoto), Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Amend, Simon Kalolo (kulia), Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Jiji hilo, Swalehe Msechu (wa tatu kushoto) na wanafunzi kutoka baadhi ya shule za msingi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askofu Malasusa akemea wazazi kutowajibika malezi ya watoto

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, amekemea tabia ya baadhi ya wazazi kuwaacha watoto wajilee kama wanyama na ndege, hivyo kusababisha kukosa maadili mema katika jamii.

Dk. Malasusa ambaye ni Mkuu wa KKKT Mteule, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ibada ya Sikukuu ya Mikaeli na Watoto, iliyofanyika katika Usharika wa KKKT Mtoni, Dar es Salaam.

"Kuanzia leo (Oktoba Mosi), kila mtu amwone mtoto wa Tanzania ni wake. Bahati mbaya wazazi tuko busy (tuna kazi nyingi) kuwatafutia watoto shule nzuri, nguo nzuri na chakula kizuri na kuwafundisha maadili mema na jinsi ya kuishi," alisema.

Alisema mtoto mdogo anamwamini sana mzazi wake na imani kwake ni kitu kikubwa sana, hivyo wazazi wana wajibu wa kuwalea katika msingi wa kuwajengea imani badala ya kuwaacha wajilee au kulelewa na watu wengine.

"Niliingia supermarket (duka kubwa la mahitaji mbalimbali) nilikuwa nafuata betri. Nilikuwa na mwanangu, nilipofika mle, akachukua toroli. Akiona 'apple' anachukua, mmoja wa wahudumu akamuuliza 'how you' (hujambo), unakwenda kulipa hivi vyote, akajibu niko na baba. "Niliposikia hivyo nikatoa hela zisizo zangu nikalipa kujenga imani kwa mtoto," alisema.

Askofu Malasusa alisisitiza kuwa watoto wanatakiwa kupata malezi mema ambayo yatawasaidia kuwajenga katika imani ya kumjua Mungu na kuishi katika misingi bora.

Alitoa mfano wa baadhi ya kinababa kuitwa na watoto wao uncle (mjomba) kwa sababu hawajui kama ndio wazazi wao kutokana na kukosa muda wa kukaa nao zaidi ya wale wanaowalea na waliozoea kuwaona mara kwa mara.

"Kinababa mnaweza kuitwa 'uncle' na watoto kwa sababu hawawajui. Mungu ametupa watoto tuwafundishe msingi mzuri wa watoto ni malezi ya baba na mama. Watoto ambao hawajapata malezi ya wazazi atakuwa mkorofi hadi kanisani," alisisitiza Malasusa.

"Hatuwezi kuwaacha watoto kama wanyama. Lazima watoto tuwalete kwa Yesu kwa sababu ni kimbilio letu. Tuwafundishe maadili mema na utoaji michango kanisani kwani huanzia nyumba ambako mtoto huwaona baba na mama wanatoa michango kanisani, hivyo kuiga mfano huo," alisema.

Malasusa aliwavunja mbavu waumini katika ibada hiyo alipoesema alipokuwa anatumika katika usharika huo miaka kadhaa iliyopita, mtoto mmoja alitoa sadaka ya noti na kumwambia mzazi wake amezoea kumpa sarafu.

Askofu Malasusa alisema kitendo hicho cha wazazi kilimjengea mtoto huyo imani kuwa fedha za sarafu ndizo zinapaswa kutolewa kama sadaka kanisani badala ya noti.

Aliwakumbusha wazazi kuwaombea watoto wanapokwenda shuleni na wale walioko mbali nao kwa kuwa wanahitaji upendo na ulinzi wa Mungu.

"Lazima tuwaombee watoto wetu. Wazazi wanaojua hawawaachi watoto wao waende shuleni bila kuwawekea mikono hata wakiwa mbali, ndiyo maana katika amri zake anasema waheshimu baba na mama yako," alisisitiza.

# NDUMBARO ARIDHISHWA UKARABATI UWANJA MKAPA

Na Saada Akida

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, ameridhishwa na kasi ya ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambao umebaki asilimia 30 kabla ya kukamilika kuelekea mechi ya ufunguzi ya michuano ya African Football League (AFL), Oktoba 20, mwaka huu.

Waziri huyo aliambatana na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Gerson Msigwa, kufanya ukaguzi wa uwanja huo jana, ambao utaanza kutumika rasmi kwenye mechi ya ufunguzi ya AFL kati ya Simba na Al Ahly ya Misri.

**Akizungumza baada ya ukaguzi, Msigwa alisema yapo mambo ambayo yanatakiwa kukamilishwa kabla ya ufunguzi wa michuano hiyo ili kukidhi mahitaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), na tayari kazi hiyo imefikia kwa asilimia 70.**

Alisema wengi watakuwa wanakumbuka moja ya changamoto kubwa zilizosababisha kuanza hekaheka kubwa ya kukarabati uwanja huo ilikuwa ni taa za uwanjani, ambazo mkandarasi anaendelea kufunga taa mpya.

"Ndani ya siku mbili kazi hii itakuwa imekamilika, kwahiyo kwa upande wa taa hatutakuwa na shida, tutakamilisha ndani ya muda tuliowapa, waziri (Ndumbaro), ametoa maelekezo kazi hiyo imalizike mapema zaidi ya muda uliopangwa ili Wakaguzi wa Shirikisho la Soka Afrika watakapofika kati ya kesho (leo) na keshokutwa (kesho), tuwe tumekalisha.

"Watakuja hapa nchini kwa ajili ya ukaguzi wa maendeleo ya uwanja huu kuwa imara kabla ya ufunguzi wa michuano ya AFL kati ya Simba na Al Ahly, utakaochezwa Oktoba 20, mwaka huu," alisema Msigwa.

Aliongeza kuwa timu ya wizara imepiga kambi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuona kila kitu kinakwenda sawa kwa muda uliopangwa kuhakikisha hakuna kinachokwama.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (katikati), akisalimiana na Balozi wa Uturuki hapa nchini, Dk. Mehmet Gulluoglu, jijini Dar es Salaam jana, ambapo walifanya mazungumzo na kukubaliana kushirikiana katika eneo la utamaduni na michezo. Kulia ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Gerson Msigwa. **MPIGAPICHA WETU**

# Karigo amwanika rasmi Mwakinyo

Na Saada Akida

MKURUGENZI wa Kampuni ya Waandaji wa Ngumi za Kulipwa nchini (PAF Promotion), Godson Karigo, atoa sababu mbili ambazo zimekwamisha, Bondia Hassan Mwakinyo, kutopanda ulingoni Ijumaa iliyopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Karigo aliitaja sababu ya kwanza ya pambano hilo kutokufanyika ni kutokana na vitendo vya bondia huyo kuingilia majukumu ya waandaji kwa kutafuta wapinzani wa kucheza nao akiwamo Bondia, Rayton Okwiri wa Kenya, lengo lake likiwa ni kupata malipo ya ziada ('cha juu').

Hivi karibuni kulitokea sintofahamu kati ya Mwakinyo na Kampuni ya PAF, ambapo bondia huyo alitakiwa kucheza Septemba 29, mwaka huu, dhidi ya bondia, Julius Indongo kutoka Namibia, kuwania mkanda wa Ubingwa wa IBA katika pambano la raundi 12 uzito wa kati.

Karigo alisema pambano hilo halikuweza kufanyika kwa sababu ya tabia za bondia huyo kuwapangia waandaji bondia anayetaka kupigana naye, hivyo kuleta ugomvi wa nje kwenye kazi.

Alisema Mwakinyo alikuwa na ugomvi na mmoja wa wadhamini wenza ambao ni kampuni ya waandaji wa ngumi wakiwa wametoa fedha pamoja na mabondia wao kuja kucheza pambano la utangulizi jambo ambalo hakulitaka.

"Kama waandaaji tulifanya majukumu yetu ya kuendelea kutafuta wadhamini, bahati nzuri alijitokeza promota mmoja maarufu Mafia Promotion, kumbe wana maugomvi yao huko kwao Tanga na alitaka mabondia wa promota huyo asipande hata mmoja ulingoni.

"Na tulishamweleza kwamba hawezi kutupangia mabondia ambao watapanda ulingoni katika mapambano ya utangulizi kwa sababu ya ugomvi wao wa nje," alisema Karigo.

Aliongeza kuwa Mwakinyo alikataa mpinzani ambaye ana viwango na kumleta Okwiri ambaye alitaka tumpe dola 9,000 akiwa tayari ameshakubaliana naye, bila ya kushirikisha waandaji.

"Kwa sababu Mwakinyo alikuwa akilazimisha huyo bondia tumpe mkataba wa dola 9,000 jambo ambalo haikuwa bajeti yetu, bajeti yetu ilikuwa dola 5,000, lakini baada ya kufuatilia Okwiri na kumtumia mwamuzi wa hapa nchini, Emmanuel Mrundwa, aliyekuwa na safari ya kwenda Nairobi.

"Tulimuomba Mrundwa kuwasiliana na Shirikisho la Ngumi la Kenya na kufanikiwa kupata taarifa za Okwiri na kusaini mkataba wa bajeti yetu, baada ya Mwakinyo kusikia kuwa tumempa bondia huyo na kusaini mkataba kwa makubaliano ya dola 5,000 alimpigia simu kutaka kumkata dola 4,000," alisema Karigo.

Alisema kitendo cha Okwiri kuambiwa na Mwakinyo atamkata dola 4,000, ndipo akaamua kutoa taarifa kuwa ameumia na kuletewa Indongo aliyekubaliana naye, lakini ghafla alikataa kupanda ulingoni pasipo taarifa rasmi kwa maandishi.

# Taifa U-18 waitwa 43 kujiandaa na CECAFA

Na Adam Fungamwango

JUMLA ya wachezaji 43 wameitwa kuunda kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanaume chini ya miaka 18 (U-18), kitakachoingia kambini Ijumaa wiki hii kwenye Kituo cha Ufundi cha TFF, Mnyanjani, Tanga, kujiandaa na mashindano ya CECAFA yatakoyofanyika Kenya baadaye mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), imeeleza kikosi hicho kitaendelea na mazoezi kabla ya kufanyika mchujo baadaye kwa ajili ya kuwapata wachezaji watakaosafiri kwenda nchini Kenya kwa ajili ya mashindano hayo.

Wachezaji waliochaguliwa kuunda kikosi hicho ni ni Antony Remi, Idd Salim, Ashraf Kibingu, Ismail Omary, Mashon Upondo, Ally Hassan, Fales Mkude, Ally Mohamed, Cyprian Kachwele na Gaby Joseph wote kutoka Azam FC, Bruno Natal, Hijja Shamte, Yassin Salehe, Said Naushad na Misheto John, hao wanatoka klabu ya Kagera Sugar.

Wengine ni Jonathan Scavian, Usack Emmanuel, Elius Frank, Idrissa Rashid, Hamisi Ismail na Daruwesh Rashid kutoka Klabu ya Simba, Hussein Adam, Lameck Lawi, na Bakari Selemani kutoka Coastal Union, Amiri Mbuyi wa Geita Gold, Zacharia Petro kutoka Mbeya City, Ashraf Aboubakar wa Malindi ya Zanzibar, Aboubakar Lubutile wa Kipanga ya Zanzibar, Sharifu Wilson na Ahmed Papino kutoka African Lyon.

Wachezaji wengine waliochaguliwa kuunda kikosi hicho ni Ali Sadiki, Mohamed Salum, wanaoichezea Yanga, Abdul Mandwanga wa Namungo, Sylvester Otto wa Ruvu Shooting, Idd Kichindo wa Prisons, Benjamin William wa Alliance FC, Herry Kiabo kutoka KMC, Ramadhani Othman wa Mashujaa, Omari Mvungi wa Nantes ya Ufaransa, Bryan Gerald na Mohamed Saad.

Wakati huohuo kikosi cha Timu Taifa ya Wanawake chini ya miaka 20, kinatarajia kushuka dimbani Jumapili kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es salaam dhidi ya Djibouti katika mechi ya kusata tiketi ya Kombe la Dunia.

Kwa mujibu wa TFF, mechi ya mkondo wa pili itachezwa hapa hapa nchini, kwenye uwanja huo huo Oktoba 11, mwaka huu.

ZISIKUPITE

## NETO KUMRITHI SALAH

LIVERPOOL ina nia ya kumsajili winga wa Wolves na Ureno, Pedro Neto, 23, ikiwa mshambuliaji wa Misri Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31, ataondoka msimu ujao. ***(Foobal Transfers)***

## KLABU NYINGI ZAMTAKA

KLABU za Arsenal, Aston Villa na Atletico Madrid pia zinawania kumsajili Pedro Neto. ***(90mins)***

## HAG KUSAJILI WENGI

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amewekea nia ya kutaka kusajili wachezaji kadhaa Januari mwakani. ***(Football Insider)***

## INACIO KWENYE RADA

BEKI wa Sporting Lisbon na Ureno, Goncalo Inacio, yupo kwenye rada za Manchester United, huku United wakituma wasaka vipaji wao kumfuatilia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Sun)***

## AFURAHIA LEVERKUSEN

MKURUGENZI wa Michezo wa Bayer Leverkusen, Simon Rolfes, amesema kocha Xabi Alonso, 41, ana furaha katika klabu hiyo ya Ujerumani baada ya kiungo huyo wa zamani wa Liverpool kuhusishwa na tetesi za kuchukua mikoba ya Carlo Ancelotti kule Real Madrid. ***(Mail)***

## ROQUE ATAKIWA BARCA

BARCELONA inapania kumjumuisha mshambuliaji wa Athletico Paranaense na Brazil, Vitor Roque mwenye umri wa miaka 18, katika klabu hiyo Januari badala ya Julai huku Mkurugenzi wa Michezo, Deco akipanga kusafiri hadi Brazil wakati wa mapumziko yajayo ya kimataifa. ***(Goal)***

## EVERTON WASIWASI KIBAO

WASIWASI mpya umeibuliwa juu ya wamiliki wapya watarajiwa wa Everton 777 Partners, baada ya Klabu ya Vasco da Gama ya Brazil, klabu yake nyingine, kushindwa kulipa malipo ya uhamisho wa wachezaji watatu uliogharimu jumla ya pauni milioni 4.5. ***(Guardian)***

## BERALDO AWINDWA LIVER

LIVERPOOL inamtaka beki wa kati wa Brazil, Lucas Beraldo, 19, na wametuma maskauti kumfuatilia akichezea Sao Paulo mara kadhaa. ***(90mins)***

## BOWEN MKATABA MPYA

KLABU ya West Ham inajadiliana na winga wa England, Jarrod Bowen, 26, kuhusu mkataba mpya huku Liverpool ikionesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Football Insider)***

## WHITE, ARSENAL WAJADILI

ARSENAL imeanza kujadiliana na beki wa England, Ben White, 25, kuhusu mkataba mpya, licha ya mchezaji huyo kubakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake unaomfanya alipwe mshahara wa pauni 120,000 kwa wiki. ***(Mail)***

## CRISTANTE AMULIKWA SAUDIA

KLABU ya Klabu Al Nassr ya Saudi Arabia ina mpango wa kumsaka kiungo wa AS Roma, Bryan Cristante mwenye umri wa miaka 28, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Calcio Mercato)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RATCLIFFE KUSITISHA KUINUNUA MAN UTD

**MANCHESTER,** England

Mashabiki na wafuasi wa klabu hiyo wameandamana wakitaka iuzwe jumla...

BILIONEA Sir Jim Ratcliffe anafikiria kuachana na mpango wake wa kuinunua Manchester United kwa sababu anatakiwa kuchukua hisa chache - jambo ambalo litaiacha familia ya Glazer kuwa na udhibiti mkubwa wa klabu hiyo.

Katika hali ya mshtuko ambayo bila shaka itachochea hasira miongoni mwa mashabiki wengi wa United, bilionea huyo wa kemikali za petroli anatafakari juu ya mabadiliko ya mbinu katika jaribio la kuvunja mkwamo katika kile ambacho kimekuwa ni mchakato wa kuchosha ambao sasa unakaribia mwezi wake wa kumi.

Msemaji wa Ratcliffe alikataa kutoa maoni yoyote, lakini inafahamika kuwa moja ya chaguzi zilizokuwa zinaangaliwa ni ununuzi wa asilimia 25 ya hisa za United.

**Hiyo inaweza kuleta kiasi cha karibu pauni bilioni 1.5 kwa familia ya Glazers, ambao walilipa pauni milioni 800 mwaka 2005 kuinunua klabu hiyo.**

Bei ambayo familia ya Glazer inaitaka kwa sasa ili kuiuza klabu hiyo ni pauni bilioni sita, lakini bado imeonesha nia ya kutotaka kuiuza kwa hisa zote 100.

Mashabiki na wafuasi wa Man United tayari wameandamana dhidi ya wamiliki wa sasa na wametaka iuzwe jumla.

Kwa mujibu wa Sky News, ambao walitoa habari za maendeleo ambayo vyanzo vilithibitisha baadaye kwa Mail Sport, ofa kama hiyo ingemfanya Ratcliffe kuwa na udhibiti mdogo kwa timu hiyo.

Mpinzani mkuu wa Ratcliffe, Sheikh Jassim Bin Hamad Al Thani, aliwasilisha ombi lake la mwisho la kuinunua moja kwa moja klabu mnamo Mei.

Mail Sport inaelewa kuwa raia huyo wa Qatar bado amejitolea kuitwaa klabu hiyo kwa asilimia 100.

# HABARI MICHEZO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,159,5

MECHI KALI
IHEFU FC
VERSUS
YOUNG AFRICANS
1 | 8.69
X | 4.44
2 | 1.33

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Adam Cheyo - 0654 252 XXX
2. Msitafa Mole - 0655 951 XXX
3. Said Yame - 0672 662 XXX
4. Clement Kileng'a - 0677 771 XXX
5. Mwanaidi Makoti - 0679 680 XXX
6. Elpidius Pius - 0711 475 XXX
7. Schola Chenjele - 0715 407 XXX
8. Philibet Kalokola - 0717 356 XXX
9. Emanuel Haule - 0717 901 XXX
10. Asha Mmasa - 0718 358 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



## POCHETTINO: CUCURELLA ATAINGIA KIKOSI CHA KWANZA

**LONDON** England

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Mauricio Pochettino, anapanga kumjumuisha Marc Cucurella kwenye kikosi cha kwanza ambacho bado kinatafutwa msimu huu.

Cucurella aliwasili Stamford Bridge kutoka Brighton & Hove Albion msimu uliopita wa majira ya joto kwa pauni milioni 55, huku kukiwa na nyongeza ya ada hadi pauni milioni 62.

Kama wachezaji wenzake wengi wapya, Mhispania huyo alitatizika Chelsea ilipomaliza nafasi ya 12, ikipitia kwa makocha wanne kabla ya mwisho wa msimu wa 2022/23.

Baada ya kutochaguliwa na kocha mpya Pochettino kwa mechi tatu za ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu, 90min iliripoti kuelekea mwisho wa dirisha la usajili la majira ya joto kwamba Manchester United walikuwa wameanzisha mazungumzo na Chelsea kuhusu kumnunua kwa mkopo Cucurella.

Hata hivyo, Cucurella alitajwa katika kikosi cha kwanza cha 'Blues' kwenye ushindi wa mechi ya Carabao raundi ya pili dhidi ya AFC Wimbledon.

Baadaye Man United ikachagua kumsajili Sergio Reguilon kwa mkopo kutoka Tottenham Hotspur badala yake.

Mechi nyingine pekee ya Cucurella msimu huu ni ushindi wa bao 1-0 dhidi ya timu yake ya zamani ya Brighton katika raundi ya tatu ya Kombe la Carabao wiki iliyopita na bado hajacheza dakika hata moja kwenye Ligi Kuu msimu huu.



## Okocha ampa neno Chukwuez

**MILAN,** Italia

JAY-Jay Okocha anaamini Mnigeria mwenzake, Samuel Chukwueze, atapata mafanikio makubwa zaidi akiwa na Klabu ya AC Milan.

Chukwueze mwenye umri wa miaka 24, alijiunga na 'Rossoneri' hao msimu wa majira ya joto baada ya misimu mitano ya kuvutia akiwa na Villarreal ya Hispania.

Winga huyo amejumuishwa taratibu katika timu ya Stefano Pioli hadi sasa, huku mechi sita kati ya saba za Serie A akitokea benchi kabla ya mechi ya Jumatano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund.

Lakini mshambuliaji wa zamani wa Nigeria, Okocha anaamini kuwa mchezaji huyo wa kimataifa ana kila kitu kuweza kufanya vema pale San Siro.

Okocha aliiambia LiveScore: "Amekuwa bora katika miaka michache iliyopita.

"Amekabiliwa na changamoto mpya na yote ni kuhusu jinsi anavyoweza kuzoea haraka. "Lugha ni muhimu kila wakati kwa sababu ni vizuri kuwa na uwezo wa kuwasiliana, lakini kipaji chake haina shaka.

"Nadhani ni nyongeza
kwa timu ya Milan na sina
ka kwamba atafanya vizur

Alipoulizwa kama
wachezaji wa sasa wan
kumbusha yeye mweny
Okocha mwenye umri
miaka 50, alisema: "Sawa,
hani mambo yamebadilik
vigumu kwa wachezaji
kujieleza.

"Unaweza kusema kwa
labda Kylian Mbappe
onekana kusisimua, pa
na Kevin De Bruyne na R
Leao kutoka AC Milan pia.

"Mbali na hayo, ni vig
kwangu kuchagua mmoja

## HABARI MICHEZO

# 574,731/-

# GOMES WA SIMBA KUTUA NCHINI KUINOA SINGIDA FG

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Singida Fountain Gate FC, umekamilisha makubaliano na aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, kuja kukinoa kikosi cha timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Gomes alionekana Misri juzi kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika kati ya Future FC na Singida Fountain Gate FC, akiwa miongoni mwa watazamaji walioko jukwaani.**

Taarifa za uhakika zilizofikia Nipashe jana kutoka chanzo chetu cha uhakika ndani ya timu hiyo, tayari Gomes amekubaliana na uongozi wa Singida Fountain Gate FC na muda wowote atasaini mkataba wa kukinoa kikosi hicho katika michezo ya Ligi Kuu na michuano mingine.

Chanzo hicho makini kilieleza kuwa uongozi umeona Gomes anastahili kuja kuchukuwa nafasi ya Ernst Middendorp aliyeondoka kutokana na kutokuwa na maelewano mazuri na waajiri wake na timu kuwa chini ya Mkurugenzi wa Ufundi, Ramadhan Nsanzwirimo.

"Mazungumzo yamekamilika kilichobakia ni kusaini mkataba na kumtambulisha rasmi kwa sababu timu ilipokuwa Misri, Gomes alikuwapo akiangalia mchezo huo ili kuangalia timu yake hiyo mpya kabla ya kuanza kuinoa," kilieleza chanzo chetu.

Nipashe lilimtafuta Ofisa Habari wa Singida Fountain Gate FC, Hassan Masanza, ambaye alikiri kuwapo kwa mazungumzo na baadhi ya makocha akiwamo Gomes kwa ajili ya kuona nani anakuja kuwa kocha mkuu.

"Kila mtu anaelewa nafasi ya kocha mkuu ipo wazi na viongozi wako kwenye mazungumzo na makocha mbalimbali, kikubwa tunaangalia mwalimu anayeifahamu soka la Tanzania na atakayeweza kutupelekea kimataifa kwa msimu ujao," alisema Masanza.

Aliongeza kuwa baada ya kufanikiwa kumpata kocha wanayemhitaji na kufika vigezo vyao, wataweka wazi na kwamba kwa sasa timu inaendelea kuwa chini ya Nsanzwirimo hadi hapo atakapopatika kocha mkuu.

Kikosi cha Singida Fountain Gate FC, tayari kimewasili Manungu, Turiani mkoani Morogoro tayari kwa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Mtibwa Sugar utakaopigwa kesho katika Uwanja wa Manungu Complex.

## Yanga SC kuivaa Ihefu

INATOKA UK. 24

ni mwingine tofauti, timu hii ni tofauti siyo ile ya msimu uliopita ina baadhi ya wachezaji wengine na benchi la ufundi lililobadilika kwa hiyo tunaamini kwamba safari hii tuna kikosi bora zaidi, imara ambacho kinaweza kuleta furaha kwa mashabiki wetu kama ambavyo imekuwa kawaida yetu kwa msimu mzima," alisema Harrison.

Nahodha Msaidizi wa Yanga, Dickson Job, amesema kwa kushirikiana na wachezaji wenzake, wataendeleza ushindani kwenye mechi hiyo ili kuipa timu matokeo mazuri.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunapata ushindi katika mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa," alisema Job.

Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, yeye amesema wataingia na mkakati wa kuwazuia viungo wa Yanga ili wasiwalishe kwa urahisi mastraika wao, lakini hatotumia mfumo mmoja, badala yake atakuwa akibadilika kutokana na mchezo unavyoendelea.

"Sisemi kama nitapaki basi au tutapishana, hiyo itategemea na jinsi mchezo unavyokwenda, lakini pia unapocheza na timu kama Yanga inawezekana wasiwe na makosa, hivyo kazi kubwa ni kuwalazimisha wafanye makosa ili tuyatumie," alisema.



Didier Gomes Da Rosa

## *Simba yatoa msimamo hatima ya Robertinho*

INATOKA UKURASA 24

kikosi hiki kitawashangaza watu," alisema Robertinho.

Alisema ana wiki mbili za kujiandaa kwa ajili ya mashindano ya kimataifa ya African Football League (AFL), hivyo atazitumia kurekebisha mapungufu aliyoyaona kwenye michezo miwili ya kufuzu hatua ya makundi dhidi ya Power Dynamos.

"Lazima tuimarishe uwezo wetu wa kukaba pale tunapokuwa hatuna mpira, tuongeze kazi wakati wa kushambulia ni mambo ambayo tunayafanyia kazi," alisema Robertinho.



## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/10/23 | 19:30 | Mallorca vs Valencia | 2.45 | 3.05 | 2.90 |
| 02. 07/10/23 | 19:30 | Werder Bremen vs Hoffenheim | 2.70 | 3.65 | 2.29 |
| 03. 07/10/23 | 22:00 | Reims vs Monaco | 2.60 | 3.55 | 2.42 |
| 04. 08/10/23 | 15:15 | FC Lugano vs Servette Geneva | 2.12 | 3.45 | 2.80 |
| 05. 08/10/23 | 16:00 | Frosinone vs Verona | 2.26 | 3.30 | 3.00 |
| 06. 08/10/23 | 16:00 | Lazio vs Atalanta | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 07. 08/10/23 | 16:00 | Tanzania Prisons vs Mtibwa Sugar | 2.25 | 2.80 | 3.40 |
| 08. 08/10/23 | 16:00 | GIF Sundsvall vs IK Brage | 2.48 | 3.20 | 2.48 |
| 09. 08/10/23 | 16:00 | Brighton vs Liverpool | 2.80 | 3.80 | 2.18 |
| 10. 08/10/23 | 16:00 | Wolverhampton vs Aston Villa | 3.30 | 3.40 | 2.07 |
| 11. 08/10/23 | 16:00 | West Ham vs Newcastle | 3.00 | 3.55 | 2.14 |
| 12. 08/10/23 | 17:30 | Lausanne-Sport vs FC Luzern | 2.44 | 3.35 | 2.42 |
| 13. 08/10/23 | 17:30 | Famalicao vs Vitoria Guimaraes | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 14. 08/10/23 | 18:05 | Lens vs Lille | 2.15 | 3.45 | 3.05 |
| 15. 08/10/23 | 18:30 | Arsenal vs Manchester City | 2.70 | 3.35 | 2.43 |
| 16. 08/10/23 | 18:30 | Hammarby vs Hacken | 2.35 | 3.35 | 2.50 |
| 17. 08/10/23 | 19:30 | Alaves vs Betis | 2.75 | 3.10 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 04/10/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3462 | Egaleo Athens vs Diagoras FC | 1.93 | 3.12 | 3.83 |
| 14:30 | 2821 | Fakel vs CSKA Moscow | 3.97 | 3.52 | 1.77 |
| 15:00 | 2297 | Shkendija vs FC Struga Trim Lum | 1.57 | 3.55 | 5.48 |
| 15:00 | 4941 | Sochi vs Gazovik Orenburg | 2.16 | 3.47 | 2.86 |
| 16:00 | 5353 | Ararat Yerevan vs Pyunik Yerevan | 8.00 | 4.60 | 1.28 |
| 16:00 | 5990 | Ihefu FC vs Young Africans | 8.69 | 4.44 | 1.33 |
| 16:45 | 4425 | Dinamo Moscow vs Spartak Moscow | 2.05 | 3.67 | 2.95 |
| 17:00 | 4109 | Viby IF vs Hvidovre IF | 16.29 | 7.74 | 1.10 |
| 17:15 | 3434 | FC Krasnodar vs Nizhny Novgorod | 1.63 | 3.56 | 4.88 |
| 17:30 | 4556 | Bengaluru FC vs East Bengal | 1.52 | 4.05 | 4.86 |
| 18:00 | 2084 | Moroka Swallows FC vs Chippa Utd | 2.04 | 2.99 | 3.76 |
| 18:00 | 2168 | AL Safa (Sa) vs AL Adalh | 4.72 | 3.52 | 1.63 |
| 18:00 | 5696 | Hajer Club vs Al-Taraji Club | 2.12 | 2.97 | 3.32 |
| 19:00 | 2321 | Pisek vs Slavia Prague B | 6.65 | 5.44 | 1.29 |
| 19:00 | 5359 | Kagera Sugar vs Namungo | 2.04 | 2.95 | 3.95 |
| 19:00 | 5601 | ISA Town vs Etehad Alreef | 1.32 | 4.50 | 7.20 |
| 19:00 | 5741 | Sogndal vs Kristiansund | 1.78 | 3.79 | 3.53 |
| 19:00 | 5792 | Um Alhassam vs Qalali | 1.97 | 3.20 | 3.30 |
| 19:45 | 1160 | Atletico Madrid vs Feyenoord | 1.60 | 3.87 | 4.86 |
| 19:45 | 3802 | Royal Antwerp vs Shakhtar Donetsk | 1.79 | 3.58 | 3.98 |
| 19:45 | 4295 | St Etienne vs Dunkerque | 1.64 | 3.76 | 4.65 |
| 20:00 | 1103 | Jahn Regensburg vs Waldhof Mannheim | 2.11 | 3.46 | 3.15 |
| 20:00 | 2373 | CD Eldense vs Valladolid | 3.07 | 3.07 | 2.28 |
| 20:00 | 2931 | Preussen Munster vs Erzgebirge Aue | 1.88 | 3.63 | 3.68 |
| 20:00 | 2969 | Real Oviedo vs Huesca | 1.97 | 3.02 | 3.96 |
| 20:00 | 4023 | Unterhaching vs RW Essen | 2.32 | 3.49 | 2.76 |
| 20:00 | 4886 | Dynamo Dresden vs Hallescher | 1.50 | 4.27 | 5.62 |
| 20:00 | 5059 | Stabaek vs Ham-Kam | 2.07 | 3.46 | 3.20 |
| 20:30 | 1463 | Cape Town Spurs vs SuperSport Utd | 4.93 | 3.29 | 1.72 |
| 20:30 | 2240 | Stellenbosch vs TS Galaxy FC | 2.28 | 2.93 | 3.23 |
| 20:30 | 5788 | Richards Bay FC vs Polokwane City | 2.53 | 2.88 | 2.88 |
| 21:30 | 4422 | Magallanes vs Univ de Concepcion | 1.66 | 3.73 | 4.39 |
| 21:45 | 1489 | Welling vs Gosport Borough | 2.06 | 3.68 | 2.91 |
| 21:45 | 1765 | Swansea vs Norwich City | 2.72 | 3.26 | 2.40 |
| 21:45 | 1819 | Sunderland vs Watford | 1.94 | 3.41 | 3.56 |
| 21:45 | 2270 | Boreham Wood vs Hartlepool | 2.39 | 3.40 | 2.68 |
| 21:45 | 2574 | Leicester vs Preston | 1.45 | 4.16 | 6.34 |
| 21:45 | 5459 | Leeds vs QPR | 1.32 | 4.87 | 7.76 |
| 21:45 | 5540 | Coventry vs Blackburn | 2.02 | 3.57 | 3.17 |
| 22:00 | 1305 | Porto vs Barcelona | 3.76 | 3.67 | 1.81 |
| 22:00 | 1891 | Celtic vs Lazio | 2.76 | 3.41 | 2.30 |
| 22:00 | 2157 | RB Leipzig vs Manchester City | 4.36 | 3.86 | 1.66 |
| 22:00 | 3076 | Red Star Belgrade vs BSC Young Boys | 2.08 | 3.47 | 3.12 |
| 22:00 | 3178 | Newcastle vs Paris St Germain | 2.47 | 3.46 | 2.52 |
| 22:00 | 5179 | Borussia Dortmund vs AC Milan | 2.33 | 3.41 | 2.72 |
| 22:00 | 5425 | Rotherham vs Bristol City | 3.48 | 3.28 | 2.01 |
| 22:30 | 4115 | Burgos vs Leganes | 2.26 | 2.92 | 3.27 |
| 22:30 | 4602 | Sporting Gijon vs Elche | 2.31 | 3.12 | 2.97 |
| 23:00 | 1760 | Vargas Torres vs Manta | 2.16 | 3.06 | 3.21 |
| 23:00 | 2688 | 9 De Octubre FC vs Imbabura Sporting Club | 2.37 | 3.26 | 2.70 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatano Oktoba 4, 2023
Nipashe




Gomes wa Simba kutua Singida FG UKURASA 23

# Simba yatoa msimamo hatima ya Robertinho

## ●●● Naye asema atawashangaza wengi lakini...

**Saada Akida na Faustine Feliciane**

LICHA ya kuzuka baadhi ya mashabiki wanaopiga debe Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira atimuliwe, huku ikisambaa taarifa kuwa tayari 'amepigwa chini', uongozi wa klabu hiyo umeibuka na kusema una imani kubwa na Mbrazili huyo na haina mpango wowote wa kumwondoa ndani ya benchi hilo la ufundi kwa kuwa bado yupo kwenye malengo yao.

**Kelele za wasiomtaka Robertinho zilikuja baada ya kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mbinde kwa faida ya bao la ugenini, kutokana na sare ya mabao 2-2 ugenini dhidi ya Power Dynamos ya Zambia kisha sare ya bao 1-1 hapa nchini, mechi zote Simba ikitokea nyuma na kusawazisha.**

Pamoja na matokeo hayo, huku pia akiwa hajapoteza mechi yoyote ya Ligi Kuu wala kutoka sare, wanadai hawafurahishi na kiwango kinachooneshwa na wachezaji wao, wakitaka soka 'biriani' (soka la kuvutia).

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema wanaimani na kocha Robertinho kwa sababu yuko kwenye malengo yao na hakuna alichokipoteza na tayari timu iko hatua ya makundi.

Alisema, "Robertinho bado ataendelea kukinoa kikosi cha timu yetu hadi mkataba wake utakapofikia tamati kwa sababu bado yuko kwenye malengo yetu na hajapewa pa kuanzia ndani ya uongozi.

"Hakuna ukweli kuwa Robertinho, kuna kiongozi aliyempa mtihani wa mechi ya Tanzania Prisons kuwa akipoteza ndio basi, kocha bado yupo kwa sababu hajatoka nje ya malengo yetu, tumefuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Ahmed.

Alisisitiza kuwa tayari kocha huyo yuko kwenye msafara wa benchi la ufundi na timu iliyosafiri kwenda Mbeya kwa ajili ya kusaka pointi tatu katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Kikosi cha wachezaji wetu kimeondoka leo (jana) kasoro Luis Miquissone ni majeruhi, hatakuwa sehemu ya mchezo huo ataambatana na Henock Inonga, Aubin Kramo na Aishi Manula ambao nao wako chini ya uangalizi wa daktari kutokana na majeraha yao," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa kikosi kipo imara na wanaenda Mbeya kwa ajili ya kusaka pointi tatu muhimu katika mchezo huo dhidi ya Tanzania Prisons utakaochezwa kesho.

Kwa upande wa Robertinho, amesema licha ya maneno anayoyasikia juu ya aina ya uchezaji wa kikosi chake, ana uhakika atawashangaza wale wanaoisema vibaya Simba kwa kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho ambaye yupo Mbeya kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu kesho dhidi ya Tanzania Prisons, alisema kama kocha anaamini ana timu nzuri inayompa matokeo, hivyo hana hofu na kikosi chake.

"Siwezi kukataa yapo mapungufu kidogo tunayotakiwa kuyafanyia kazi ili kuwa bora zaidi, hilo nalifanyia kazi, lakini niseme tu

INAENDELEA UKURASA 23



Robertinho

# Yanga kuivaa Ihefu kwa tahadhari

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

MABINGWA Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga, leo wanatarajiwa kucheza mechi ya kwanza msimu huu wakiwa ugenini, watakaposhuka katika Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Ubaruku, Mbeya kucheza dhidi ya timu ngumu ya Ihefu FC.

Yanga itaingia kwenye uwanja huo ikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya timu hiyo, Novemba 29, mwaka jana katika mechi ya Ligi Kuu msimu uliopita iliyomaliza mfululizo wao wa kutopoteza mechi 49.

Mabingwa hao walicheza mechi zao tatu za mwanzo nyumbani, wakitumia Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam dhidi ya KMC ikishinda mabao 5-0, JKT Tanzania ikishinda tena kwa idadi hiyo hiyo ya mabao na Namungo ikishinda bao 1-0.

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema anatarajia kuwa utakuwa mchezo mzuri na mgumu kwa sababu mwanzo wa ligi timu nyingi zinakuwa zipo vizuri, lakini pia kila timu inapocheza na bingwa mtetezi inajaribu kucheza mchezo bora zaidi ya siku zote.

"Tunafahamu kwamba ni mwanzo wa ligi na kila timu iko kwenye nafasi nzuri na kujaribu kufanya vizuri zaidi inapokutana na bingwa mtetezi, ni sisi sasa kuhakikisha tunaendelea kucheza kwa kiwango cha juu na nina imani tutaendelea kufanya hivyo ikiwa ni pamoja na kufanya vizuri kwenye mchezo wetu huu," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Meneja wa Klabu hiyo, Walter Harrison, alisema Yanga iliyofungwa na Ihefu msimu uliopita siyo hii ya sasa.

"Tuko tayari kwa mchezo husika na kama utakumbuka Ihefu imekuwa na timu nzuri tangu msimu uliopita, walicheza vizuri sana na hatukuweza kupata matokeo mazuri kwenye uwanja wao, lakini huu mchezo

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042